# Mikakati Endelevu ya Utetezi wa Elimu Mjumuisho kwa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu

**Moduli ya**

# 4




## Muongozo wa mwezeshaji

Umetayarishwa kwa ajili ya:

Jumuiya ya MECP-Z na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu

The Norwegian Association of Disabled

Umetayarishwa na:

Enabling Education Network

NAD – The Norwegian Association of Disabled

MADRASA EARLY CHILDHOOD PROGRAMME

EENET

Inclusive Learning Approach

SHIJUWAZA

[maelezo ya picha]: Kuna watu watano waliokaa katika chumba. Kuna kalenda ukutani. Upande wa kulia kuna mtu aliyevaa kwa unadhifu ambae amekaa nyuma ya dawati ambalo juu yake kuna rundo la karatasi. Kwenye meza yake pana maandishi yanayosomeka ‘Afisa Elimu Wilaya’. Anasikiliza kwa umakini. Mbele yake kuna watu wanne waliokaa juu ya viti wakimuelekea Afisa elimu. Kando yake kuna mwanamke aliyevaa kwa unadhifu akiwa ameshika fimbo ndefu nyeupe. Anazungumza kwa ishara akimueleza jambo fulani Afisa. Ameshika nyaraka rasmi za serikali zikiwa na nembo ya serikali. Karibu yake kuna kijana mdogo wa kiume aliyeshika fimbo nyeupe pamoja na mtu mzima mwanamme na mwanamke. Wanatabasamu.]

Kazi hii imepewa kibali chini ya Creative Commons Attribution Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. Ili kuona leseni ya kopi hii, tembelea http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/

# Yaliyomo


Utangulizi.......................................................................................................4

Kipindi cha 1: Kupitia moduli ya 1–3 na kuutambulisha Muongozo wa Utetezi..5

Kipindi cha 2: Kueleza mafanikio yetu katika utetezi wa elimu mjumuisho........9

Kipindi cha 3: Majukumu ya Jumuiya za watu wenye ulemavu katika kutetea elimu mjumuisho ....................................................................................13

Kipindi cha 4: Mikakati na fursa za kuendeleza kazi ya utetezi katika elimu mjumuisho.....................................................................................................20

Nyenzo nambari 1.1: Kadi za mapitio ya elimu mjumuisho ..............................39

1.1b: Aina 6 za vikwazo vya elimu elimu mjumisho.........................................42

Nyenzo namabri 1.3: MUONGOZO WA UTETEZI: Kusaidia jumuiya za watu wenye ulemavu kufanya utetezi wa elimu mjumuisho ....................................68

Nyenzo nambar 2.1: Muongozo wa kuandaa mabango/kupeana taarifa kuhusu mafanikio.........................................................................................................71

Nyenzo nambari 3.1: Majukumu ya Jumuiya za Watu wenye Ulemavu katika Kutetea Elimu Mjumuisho...............................................................................73

Nyenzo nambari 4.2: Mikakati muhimu ya kuendeleza kazi ya utetezi katika elimu mjumuisho ............................................................................................83

Nyenzo nambari 4.4: Sehemu za maigizo zinazoonesha changamoto za uendelevu katika elimu mjumuisho ................................................................85

# Utangulizi

Moduli hii ina malengo matatu:

1. Kupeana taarifa kuhusu mafanikio na changamoto zinazohusu utetezi wa elimu mjumuisho.
2. Kufahamu na kuimarisha majukumu tofauti tunayotekeleza sisi Jumuiya za watu wenye ulemavu.
3. Kuchunguza umuhimu wa uendelevu na kukubaliana juu ya mikakati ili kuendeleza kazi ya utetezi wa elimu mjumuisho.

Moduli ya 4 inazisaidia Jumuiya za watu wenye ulemavu (JWU) pamoja na wadau wengine muhimu ili kupitia dhana za msingi na jumbe kutoka katika moduli ya 1 – 3. Hii ni pamoja na 'Muongozo wa Utetezi' ambao unajumuisha nyenzo na rasilimali kwa ajili ya kusaidia kazi ya utetezi wa elimu mjumuisho inayotekelezwa na jumuiya za watu wenye ulemavu.

Pia inatoa fursa kwa jumuiya za watu wenye ulemavu kuelezea mafanikio na changamoto katika utetezi wa elimu mjumuisho. Inawezesha Jumuiya za watu wenye ulemavu kufahamu majukumu tofauti ambayo zimetekeleza kama watetezi na jinsi gani wanaweza kuendeleza harakati hizo kupitia uzoefu wa kazi ambayo zimeshafanya.

Mwisho, moduli ya 4 inaainisha umuhimu wa uendelevu na mikakati ya kuendeleza kazi ya utetezi katika elimu mjumuisho.

## Muda wa mafunzo

Iwapo shughuli zilizomo katika moduli hii zitafanyika bila ya marekebisho makubwa, kufupisha au kurefusha, moduli hii itachukua takribani saa 14 za mafunzo. Moduli tatu ambazo zilifundishwa kwa takribani zaidi ya mwaka mmoja zitafundishwa kwa siku tatu hadi tano, kwa kutegemea na urefu wa siku za mafunzo, idadi, na urefu wa vipindi vya mapumziko, n.k.

# Kipindi cha 1: Kupitia moduli ya 1–3 na kuutambulisha Muongozo wa Utetezi

### Ujumbe mahususi

Ni muhimu kupitia jumbe mahususi na dhana kutoka katika moduli za mafunzo yaliyopita ili kuhakikisha watu wote wana uelewa sawa na wanakwenda sambamba katika mafunzo. Itasaidia pia kuharakisha ufahamu wa washiriki wapya kutoka katika Jumuiya za watu wenye ulemavu hasa kwa wale ambao ndio kwanza wamejiunga na mafunzo haya.

## Taarifa za awali kwa mkufunzi:

Kipindi hiki kinatambulisha baadhi ya 'kadi za mapitio' ambazo zinaonesha kwa picha na maelezo jumbe mahususi na dhana kutoka katika moduli ya 1 – 3. Dhamira kuu ya kadi hizi za mapitio ni kutoa nyenzo ambazo zinaweza kutumika kupitia jumbe mahususi na dhana kutoka katika mafunzo ya elimu mjumuisho ya Jumuiya za watu wenye ulemavu. Hizi zinaweza kutumiwa na SHIJUWAZA na Jumuiya za watu wenye ulemavu katika ngazi ya taifa na wilaya kama ni sehemu ya mafunzo endelevu kwa wanachama wake.

Kipindi hiki pia kinautambulisha Muongozo wa Utetezi, ambao umekusanya maudhui yote muhimu ambayo Jumuiya za watu wenye ulemavu zilijifunza ili kuziwezesha kuwa watetezi wazuri wa elimu mjumuisho.

## Katika Kipindi hiki washiriki:

- Watapitia jumbe mahususi na dhana kutoka katika moduli 1 – 3 za mafunzo ya elimu mjumuisho kwa Jumuiya za watu wenye ulemavu.
- Wataelezwa kwa muhutasari Muongozo wa Utetezi wa elimu mjumuisho kwa Jumuiya za watu wenye ulemavu.

## Shughuli nambari 1.1: Kupitia moduli 1 – 3

1 dakika 60

### Maelekezo

Waombe washiriki wakae katika vikundi vya watu 4 - 5

**Nyenzo nambari 1.1** **kadi za mapitio ya elimu mjumuisho**

Gawa seti moja ya 'kadi za mapitio ya dhana za elimu mjumuisho' kwa kila kikundi ambazo watazichanganya na kuzifunika katikati ya meza.

Kadi hizi ni pamoja na karatasi ya A4 kila moja ikiwa na picha na maelezo yanayoeleza:

a. Uwepo, ushiriki, na mafanikio
b. Aina za vikwazo vinavyozuia elimu mjumuisho
c. Sekta ya elimu – vipengele mbalimbali
d. Vikwazo vinavyohusiana katika elimu mjumuisho
e. Duara (mzunguko) la ubaguzi
f. Ushirikiano na Kamati za elimu mjumuisho za skuli
g. Jukumu la Kamati ya Elimu mjumuisho linaloiunganisha jamii na skuli
h. Mfumo wa elimu ndio tatizo na SIO mwanafunzi
i. Mkabala wa njia pacha
j. ANGALIA na TAFAKARI kabla ya KUTENDA
k. Kutambua rasilimali zilizopo katika jamii
l. Harakati kubwa na ndogo za utetezi
m. Uhamaji jumuishi huanza nyumbani
n. Majukumu ya Jumuiya za watu wenye ulemavu katika utetezi wa elimu mjumuisho

**Power Point** **Kipindi cha 1 slaidi ya 1: Shughuli nambari 1.1: Maelekezo**

Kila mshiriki katika kikundi, kwa zamu achague kadi moja, aiangalie kwa uficho, (bila ya washiriki wengine kuiona) na aeleze dhana/ujumbe mahususi ulioandikwa katika kadi hiyo kupitia 'mifano halisi' lakini ajitahidi asitaje neno lenyewe lililoandikwa katika kadi. Ili kutoa mfano wa shughuli yenyewe, fanyeni shughuli moja kwa pamoja.



[Maelezo ya picha]: Washiriki wakiwa katika picha ya pamoja Zanzibar wakijadiliana kuhusu 'kadi za mapitio ya dhana za elimu mjumuisho' na kufahamishana huku mshiriki mmoja akiandika mawazo ya kikundi.]

- Iwapo mshiriki atachagua kadi ambayo anahisi ni ngumu kuielezea, anaweza 'kuiweka' chini na kuchagua kadi nyengine.
- Baada ya dhana/ujumbe mahususi kuaguliwa kwa usahihi wanakikundi wengine wataongeza kwa kutaja mifano mingine katika tafsiri/maelezo na kujadili tofauti za ufahamu kabla ya kujadili nyengine.

## Shughuli nambari 1.2: Kutambulisha Muongozo wa Utetezi

1 dakika 40

### Maelekezo

- Inua rasimu ya kopi ya Muongozo wa Utetezi na eleza kwamba muongozo huu umeandaliwa ili kuzisaidia Jumuiya za watu wenye ulemavu (JWU) katika kazi yao ya utetezi wa elimu mjumuisho.
- Eleza kwamba Muongozo wa Utetezi umekusanya kazi zote ambazo tumekuwa tukizifanya katika kujenga uwezo wa utetezi kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita na umejumuisha mifano halisi ya kazi zilizokuwa zinafanywa na JWU.

- Onesha **PPT 3 ya Shughuli nambari 1.2: Nini maana ya Muongozo wa Utetezi?** Na waeleze washiriki dhana sahihi na isiyo sahihi kuhusu Muongozo wa Utetezi.

**Power Point** — **Kipindi cha 1 Slaidi ya 2: Nini maana ya Muongozo wa Utetezi?**

- Waombe washiriki wajigawe katika jozi na wape kila jozi kopi ya **Nyenzo 1.3: Muhutasari wa Muongozo wa Utetezi**

**Nyenzo** — **Muhutasari wa Muongozo wa Utetezi**

- Waombe washiriki kusoma kwa umakini kilichoandikwa katika Muongozo wa Utetezi. Hakikisha kwamba kila jozi ina mtu ambae anaweza kusoma muhutasari huo.
- Iombe kila jozi kujadili maswali yafuatayo (onesha PPT 4 Shughuli nambari 1.2)

**Power Point** — **Kipindi cha 1 slaidi ya 3: Kuangalia na kutafakari kuhusu Muongozo wa Utetezi**

  - **Unadhani ni sehemu ipi ya Muongozo wa Utetezi itakua muhimu zaidi kwa kazi yako ya utetezi? Kwa nini?**
  - **Kwa namna gani unaweza kuutumia Muongozo wa Utetezi ili kukusaidia kutekeleza shughuli zako za utetezi?**
  - **Unaweza kutoa mifano?**
- Wape washiriki takribani dakika 20 kujadili maswali.
- Baada ya washiriki wote kumaliza waulize iwapo kuna mshiriki yeyote ambae angependa kueleza walichokijadili. Wahamasishe washiriki kueleza mifano ya jinsi gani wanaweza kuutumia muongozo. Andika mapendekezo ya ziada kwenye chati mgeuzo.
- Mwisho waeleze kwamba tutarejea mara kwa mara katika Muongozo wa Utetezi katika vipindi tofauti na siku ya mwisho kutakua na Shughuli itakayofafanua kwa kina ‘Matumizi ya Muongozo wa Utetezi’.

# Kipindi cha 2: Kueleza mafanikio yetu katika utetezi wa elimu mjumuisho.

**Ujumbe mahususi**

Ni muhimu kukumbuka mafanikio tuliyoyapata, rasilimali zinazopatikana katika wilaya na ushirikiano ulioanzishwa ikiwa ni hatua ya awali katika kufikiria jinsi ya kuendeleza kazi yetu katika utetezi wa elimu mjumuisho.

## Taarifa za msingi kwa mkufunzi:

Kipindi hiki ni fursa muhimu kwa viongozi wa Jumuiya za watu wenye ulemavu, wanachama wa jumuiya, wazazi, na wadau wengine wa elimu kutafakari juu ya mafanikio ya Jumuiya za watu wenye ulemavu katika kutetea elimu mjumuisho.

Kwa kutafakari mafanikio yao, Jumuiya za watu wenye ulemavu zinaweza kuuliza maswali kama vile:

- **Kitu gani ambacho tumekuwa tukikifanya vyema ambacho tunapaswa kuongeza bidii zaidi (Nguvu/Uimara)**
- **Ni jinsi gani tunaweza kutumia mafanikio yetu kujiimarisha zaidi? Kuna fursa zipi zilizopo? (Fursa)**
- **Kuna mapungufu gani katika kazi yetu? Maeneo yepi tunapaswa kufanya vyema? (Udhaifu)**
- **Kuna changamoto zipi zinazokabili kazi yetu ya utetezi wa elimu mjumuisho? (Vitisho)**

Sampuli ya maswali ya hapo juu inajulikana pia kama uchambuzi wa SWOT. SWOT inawakilisha:
S = Strengths
W = Weaknesses
O = Opportunities
T = Threats

## Katika Kipindi hiki washiriki:

- ü Watatafakari mafanikio waliyoyapata katika utetezi wa elimu mjumuisho.
- ü Kujadili fursa na changamoto zilizopo katika utetezi wa elimu mjumuisho.

## Shughuli nambari 2.1:

Kutafakari kuhusu mafanikio yetu.

Uwasilishaji ngazi ya taifa: Kabla ya mafunzo kuanza ukumbi uwe umewakilishwa na Shehia (5) kwa kila Wilaya tatu, Shehia hizo ni Kikwajuni juu, Chumbuni, Kwa Wazee, Kwa Alimsha na Mchangani kwa wilaya ya Mjini vile vile, Mtende, Kizimkazi, Kajengwa, Paje and Jambiani kwa Kusini Unguja na Ng'ambwa, Shungi, Mjini Ole, Tibirinzi na Pujini kwa Wilaya ya Chakechake Pemba zikionesha mabango na nyenzo nyegine zikionesha mafanikio na changhamoto katika utekelezaji wa kazi za utetezi wa elimu mjumuisho katika wilaya zao katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Wape muongozo wa kutengeneza mabango unaopatikana katika Nyenzo 2.1 mapema kabla ya kusomesha moduli ya 4 ili jumuiya ziwe na muda wa kuandaa na kupatiwa msaada zinaouhitaji. Mabango hayo hayo yanaweza kutumika wakati mafunzo yakiendelea baadae.

**Nyenzo**

### Muongozo wa kuandaa mabango




Bango lililoandaliwa na jumuiya ya watu wenye ulemavu

[Maelezo ya picha: Picha inaonesha karatasi tofauti za chati mgeuzo zilizobandikwa ukutani zikionesha kuimarika kwa ufikiaji katika skuli na ofisi za Jumuiya za watu wenye ulemavu na Jumuyia za wazazi wa watoto wenye ulemavu]

Tafadhali waarifu washiriki kwamba kwa Shughuli ya mwanzo katika Kipindi cha 2 watahitajika kuleta visaidizi (mabango, michoro au chati mgeuzo) kwa ajili ya kuonesha kazi yao ya utetezi. Wape muda mwisho wa Kipindi hiki (dakika 15) ili kujadili visaidizi vipi vya kusomeshea wanataka kuvionesha.

**Power Point** **Maelekezo**

1 Dakika 60

- Ngazi ya taifa: Waeleze washiriki kwamba tutaoneshana mabango kwa ‘kutembelea maonesho’ ya wenzetu – na onesha (ashiria) mabango yaliyobandikwa katika kuta za ukumbi. Baadae onesha maswali yaliyoandikwa katika slaidi ya PawaPointi (Kipindi cha 2, slaidi ya 1) na waombe washiriki watafakari mabango hayo huku wakizunguka ukumbini.
- Anza katika ngazi ya shehiya: Tumia dakika 10 – 15 kuzungumzia mafanikio, changamoto zozote ulizokabiliana nazo na jinsi gani walitatua changamoto hizo.
- Toa muda kwa ajili ya maswali na ufafanuzi.



[Maelezo ya picha: Picha ya washiriki saba wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu kutoka Kusini – Unguja walipokua wakitembelea maonesho ya washiriki wengine katika warsha ya Jumuiya za watu wenye ulemavu, mmoja wa washiriki akieleza mafanikio, changamoto na namna ya kuzitatua changamoto hizo katika jamii yao baada ya mafunzo ya Moduli ya 2. Kuna washiriki wengine sita wanaotembelea onesho hilo, wakitazama na kusikiliza kwa umakini.]

- Baada ya kutembelea maonesho au kusikiliza wasilisho, waombe washiriki wakusanyike katika vikundi vya watu 4-5 ili wajadili maswali yafuatayo:

**Power Point** **Kipindi cha 2 Slaidi ya 1: Kutafakari 'mafanikio' yetu**

 - Kitu gani ambacho tumekua tukikifanya vyema ambacho tunapaswa kuongeza bidii zaidi **(Nguvu/Uimara)**
 - Ni jinsi gani tunaweza kutumia mafanikio yetu kujiimarisha zaidi? Kuna fursa zipi zilizopo? **(Fursa)**
 - Kuna mapungufu gani katika kazi yetu? Maeneo yepi tunapaswa kufanya vyema? **(Udhaifu)**
 - Kuna changamoto zipi zinazokabili kazi yetu ya utetezi wa elimu mjumuisho? **(Vitisho)**

Katika majadiliano waombe washiriki kutoka katika kila kikundi kueleza majibu yao na yaandike chini ya vichwa vya habari vifuatavyo:

| **Uimara** | **Fursa** |
|---|---|
| **Udhaifu** | **Vitisho/Changamoto** |

# Kipindi cha 3: Majukumu ya Jumuiya za watu wenye ulemavu katika kutetea elimu mjumuisho

**Ujumbe mahususi**

- Jumuiya za watu wenye ulemavu na familia zina jukumu muhimu la kutekeleza, katika jamii na ngazi ya taifa katika kutetea elimu mjumuisho.
- Majukumu hayo yapo ya aina tofauti lakini kuna majukumu matano ambayo ni muhimu zaidi. Majukumu yenyewe ni:
    - Kutumia sera kushawishi maamuzi kwa ajili ya kuleta mabadiliko.
    - Kuangalia, kukusanya na kupashana taarifa ili kukusanya ushahidi kwa ajili ya kuleta mabadiliko.
    - Kuwezesha ushirikiano ili kujenga ushirika madhubuti na mitandao kwa ajili ya kuleta mabadiliko (kati ya familia, wazazi na wanafunzi, skuli/kamati ya skuli, na watu/jumuiya katika jamii)
    - Kukuza uelewa kuhusu mabadiliko yanayohitajika kwa ajili ya elimu mjumuisho.
    - Kufuatilia na kuwezesha hatua ya mabadiliko kwa ajili ya elimu mjumuisho (katika skuli, jamii na serikali)

Jukumu ambalo jumuiya ya watu wenye ulemavu inapaswa kulitekeleza itategemea muda husika, kwa hivyo jukumu la utetezi litabadilika kwa mujibu wa hali.

## Taarifa muhimu kwa mkufunzi

Kuna sababu nyingi zinazofanya Jumuiya za watu wenye ulemavu kuwa ni taasisi sahihi za kuendesha harakati za utetezi kwa ajili ya elimu mjumuisho. Taasisi hizi ni kiungo muhimu kati ya skuli na jamii, hasa wazazi. Wanachama wao ni wanajamii pia, kwa hivyo wana ufahamu mzuri kuhusu changamoto zinazokabili jamii yao. Wanachama wao pia wana uelewa wa kutosha, kutokana na uzoefu wao, wa mambo ambayo ni muhimu kwa elimu mjumuisho, kama vile ubaguzi na unyanyapaa. Mara nyingi pia hushiriki katika vyombo mbalimbali pamoja na wawakilishi wa serikali na wafanya maamuzi wengine ambapo wanaweza kuibua mambo muhimu na kushawishi fikra za watu.

Lakini kuweza kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi ni pamoja na kufahamu jukumu hilo linahusisha nini na kuweza kutathmini wajibu gani unahitajika

katika hali tofauti. Kwa hivyo, tunapaswa kufahamu kila jukumu linahusu nini, ujuzi gani na maarifa ambayo wanachama wa Jumuiya za watu wenye ulemavu wanayahitaji ili kuweza kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi na ni wakati gani ambao utakuwa ni sahihi zaidi kutekeleza majukumu hayo. Ijapokuwa kuna majukumu mengi ya kiutetezi ambayo Jumuiya za watu wenye ulemavu zinaweza kuyatekeleza, kuna majukumu matano ambayo Kipindi hiki kitayalenga. Wakati mwengine mabadiliko yanayohitajika yatatulazimu kutekeleza zaidi ya jukumu moja.

### Katika Kipindi hiki washiriki:

- ü Watachunguza na kufahamu majukumu ya msingi ambayo Jumuiya za watu wenye ulemavu wanaweza kuyatekeleza kama watetezi wa elimu mjumuisho na jinsi gani ya kuyatekeleza ipasavyo.
- ü Kutafakari juu ya kazi ya utetezi waliofanya na jinsi gani walitekeleza majukumu haya.
- ü Kutafakari baadhi ya changamoto katika kutekeleza majukumu haya.

## Shughuli ya 3.1: Majukumu matano ya msingi ya utetezi wa elimu mjumuisho kwa jumuiya za watu wenye ulemavu

Kabla ya kipindi kuanza tengeneza mistari ya karatasi kutoka katika karatasi tatu zenye rangi tofauti za A4.

1 Dakika 60

### Maelekezo

- Wakumbushe washiriki kwamba katika Moduli ya 3 tulizungumzia majukumu ya msingi ambayo Jumuiya za Waatu wenye Ulemavu zinaweza kutekeleza ili kuzisaidia skuli kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji/mpito jumuishi.
- Waambie kwamba ijapokuwa tulizungumzia majukumu haya kwa kuhusisha wanafunzi walio nje ya skuli na uhamaji jumuishi, haya ni majukumu muhimu ambayo Jumuiya za watu wenye ulemavu zinaweza kuyatekeleza katika utetezi wa elimu mjumuisho.
- Onesha **Slaidi ya 1** na wakumbushe washiriki kuhusu majukumu matano ya msingi.

Power Point

**Kipindi cha 3 Slaidi 1: Majukumu ya msingi ambayo jumuiya za watu wenye ulemavu zinaweza kuyatekeleza.**

- Wagawe washiriki katika vikundi vitano. Hakikisha kwamba kuna uwakilishi wa makundi tofauti mf. wazazi, wanajamii katika kila kikundi.
- Wape kila kikundi karatasi ya chati mgeuzo, moja kati ya majukumu matano na picha inayolingana na jukumu hilo kutoka katika Nyenzo 3.1.

Nyenzo nambari 3.1

**Picha na majukumu ya Jumuiya za watu wenye ulemavu**

- Waombe wabandike picha yao katikati ya karatasi yao ya chati mgeuzo na andika majukumu yao chini yake (hatimae kila kikundi kina jukumu linalotofautiana na kikundi chengine)
- Gawa karatasi zenye mistari ya rangi kwa kila kikundi na hakikisha kwamba kila kikundi kina mistari michache ya rangi tofauti.
- Onesha **Slaidi ya 2** na wasomee maswali matatu.

Power Point

**Kipindi cha 3 Slaidi 2: Maswali kuhusu majukumu ya msingi**

Maswali yenyewe ni:

- **Swali la 1:** Mabadiliko gani muhimu ambayo tunaweza kuyaleta katika elimu mjumuisho kwa kutekeleza majukumu haya? (mf. Tunaweza kupitia majukumu haya kuwasaidia wazazi kufahamu haki za watoto wao)
- **Swali la 2:** Tunahitaji ujuzi gani ili tuweze kutekeleza ipasavyo jukumu hili? (mf. Tunahitaji tuwe na weledi wa kusikiliza)
- **Swali la 3:** Kuna changamoto gani ambazo huenda zikajitokeza tutakapokuwa tunatekeleza jukumu hili la utetezi? (mf. Watu wenye ulemavu katika jamii hawatoona umuhimu).

- Waeleze kwamba wanapaswa kuandika majibu yao katika karatasi. Chagua rangi moja kwa kila swali kwa hivyo watu wote waandike jibu la swali hilo katika karatasi ya rangi sawa. Kwa mfano:
  - 1 Majibu ya Swali la 1: **Mistari ya buluu**
  - 2 Majibu ya Swali la 2: **Mistari ya pinki**

o 3 Majibu ya Swali la 3: Mistari myeupe

- Andika rangi ambayo wanapaswa kuitumia kwa kila swali katika chati mgeuzo/ubao, ili kila mmoja akumbuke rangi inayotakiwa.
- Wape dakika 45 kujadili na kutoa majibu.




Mfano wa chati mgeuzo iliyojazwa ambayo inaelezea jukumu la ‘kuongeza uelewa kuhusu mabadiliko yanayohitajika katika elimu mjumuisho’

[Maelezo ya picha: Picha inaonesha karatasi ya chati mgeuzo ikiwa na picha katikati na maneno ‘kukuza uelewa kuhusu mabadiliko yanayohitajika katika elimu mjumuisho’. Kuna mistari midogo midogo ya karatasi yenye rangi tofauti – buluu, pinki, na nyeupe – ikiwa na maandishi pembezoni mwa chatimgeuzo].

- Watakapomaliza waombe kila kikundi kubandika chati mgeuzo yao ukutani na wabandike majibu ndani ya chati mgeuzo.
- Sasa waombe washiriki kuzunguka ndani ya ukumbi kuangalia majukumu tofauti na majibu kutoka katika vikundi. Hakikisha kwamba, kuna karatasi za

ziada zenye mistari ya rangi ili washiriki waweze kuongeza orodha ya majukumu wakitaka kufanya hivyo.

- Baada ya kila mshiriki kuangalia na kutafakari kuhusu majukumu matano waombe washiriki warudi katika vikundi vyao na kutafakari katika majadiliano. Unaweza kuwauliza:
    - Ilikuwa rahisi kiasi gani kufikiria aina ya mabadiliko ambayo kupitia majukumu yetu tunaweza kuyaleta na changamoto tunazoweza kukabiliana nazo?
    - Kuna jambo lolote jipya lililojitokeza katika mjadala ambalo wangependa wawaeleze washiriki wengine?
- Onesha **Slaidi ya 3** na wasomee nukta kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ya utetezi kwa ufanisi.

**Power Point**

**Kipindi cha 3 Slaidi ya 3: Mambo muhimu ya kuzingatia ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ya utetezi kwa ufanisi**

- Jukumu la utetezi ambalo tunapaswa kulitekeleza kama jumuiya ya watu wenye ulemavu litategemea tunahitaji kuona mabadiliko ya aina gani – Lakini kinachohitajika kinaweza kutofautiana katika nyakati tofauti (mf. Wakati wa UVIKO), kwa hivyo tunahitaji kila mara kufikiria jukumu gani ni bora zaidi kwa ajili ya kuleta mabadiliko tunayoyataka katika wakati husika.
- Mara nyingi mabadiliko tunayoyatarajia yatatulazimisha tutekeleze zaidi ya aina moja ya jukumu la utetezi.
- Ili tuweze kutekeleza ipasavyo jukumu la utetezi tunahitaji kuwa na ujuzi sahihi kwa jukumu husika – kwa hivyo mara nyingi tunapaswa kufikiria ujuzi tunaouhitaji ili tuweze kutekeleza jukumu ipasavyo.
- Ni kawaida kuwepo changamoto katika utekelezaji wa jukumu – lakini tunaweza kupunguza changamoto hizi kwa kufikiria ni jinsi gani tunaweza kuzitatua.

Fikiria changamoto fulani katika jamii yako ambayo jumuiya ya watu wenye ulemavu ingependa kuitetea ipasavyo halafu jaza jaduweli lifuatalo:

| | |
|---|---|
| Kipi kiini cha tatizo katika changamoto hii? | |
| Jinsi gani Jumuiya ya watu wenye ulemavu inaweza kushirikiana na watu wengine kufahamu athari na kutafuta njia za utatuzi au suluhu? | |
| Je, serikali/jamii ifanye nini kutatua changamoto hiyo? | |
| Nani ahusishwe katika kutatua changamoto hiyo? | |
| Lipi lingekua jukumu la jumuiya ya watu wenye ulemavu katika hali hii? | |

- Hitimisha Kipindi hiki kwa kuuliza iwapo kuna mshiriki yeyote mwenye swali

## Shughuli nambari 3.2: Tafakari kuhusu majukumu ambayo tumekua tunatekeleza

Shughuli hii inaweza kufanywa kwa vikundi au kwa pamoja katika mjadala na washiriki wote.

1 dakika 45

### Maelekezo

- Waombe washiriki waunde vikundi vipya au washiriki wote kama kundi moja.
- Waeleze kwamba tunakwenda kuitafakari kazi ya utetezi ambayo tuliifanya mwaka uliopita na kujadiliana kuhusu jukumu ambalo tulikuwa tunatekeleza.
- Kipatie kila kikundi karatasi ya chati mgeuzo na kalamu (iwapo wanafanya kazi katika vikundi)
- Onesha **Slaidi ya 4** na soma maswali ili washiriki wajadili katika vikundi vyao.

Power Point

**Somo 3 Slaidi ya 4: Kwa kiasi gani tumekuwa tukitekeleza majukumu yetu kwa ufanisi?**

- Maswali:
  - o Majukumu gani MAWILI ya utetezi ambayo unahisi uliyatekeleza kwa ufanisi zaidi kama jumuiya ya watu wenye ulemavu ili kuimarisha elimu mjumuisho katika wilaya yako?
    - § Kwa nini unadhani ulikua na ufanisi katika majukumu haya?
  - o Jukumu lipi la utetezi unadhani hukulitekeleza vizuri?
    - § Kwa nini unadhani hukuweza kutekeleza vizuri jukumu hilo?
- Wape kiasi cha dakika 30 kuyajadili maswali. Waombe kila kikundi kuandika majibu yao katika chati mgeuzo (au wakifanya kazi kama kundi moja, kuandika majibu yao katika chati mgeuzo mbele ya ukumbi wa mafunzo).
- Wakishamaliza waombe warudi katika nafasi zao.
- Waombe kila kikundi kuwasilisha nukta kuu zilizojitokeza. Toa muda kwa washiriki wengine kuwauliza maswali.
- Baada ya vikundi vyote kuwasilisha washukuru washiriki kwa ushiriki wao katika Kipindi hiki. Waambie kwamba kutekeleza majukumu tofauti ya utetezi kama jumuiya za watu wenye ulemavu ni sehemu muhimu sana katika kujenga na kuimarisha elimu mjumuisho Zanzibar na hivi sasa tutaangalia ni jinsi gani tunaweza kuendeleza kazi yetu ya utetezi.

# Kipindi cha 4: Mikakati na fursa za kuendeleza kazi ya utetezi katika elimu mjumuisho

## Ujumbe mahususi

Tunapofikiria uendelevu, mara nyingi huwa tunafikiria jinsi ya kuendelea kufanya shughuli za mradi na kwa hivyo, jinsi ya kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza hilo. Hata hivyo, uendelevu wa kweli ni kuwepo mabadiliko ya muda mrefu ya kimfumo na hutokea pale tu mabadiliko yanapoendelezwa katika mfumo wa elimu.

Kuna mambo mengi ambayo JWU hufanya ili kujenga uendelevu, na ni muhimu kuyatambua na kuyathamini. Changamoto iliyopo ni kujiweka kimkakati zaidi na kufikiria shughuli zipi zinahitajika ili kutatua vikwazo vinavyojitokeza mara kwa mara na mapungufu na kujenga uendelevu katika ngazi tofauti.

## Taarifa za msingi kwa mkufunzi

Njia moja ya kufahamu na kubainisha uendelevu katika elimu mjumuisho ni kufikiria mabadiliko kwa kuhusisha na vipengele vifuatavyo:

- **Mfumo wa elimu;** mabadiliko ya sera na utekelezaji.
- **Jamii:** kukuza harakati za kuongeza uelewa katika jamii na mabadiliko katika muundo wa jamii na mabadiliko ambayo yanaonesha kubadilika kwa mtazamo.
- **Jumuiya:** mabadiliko ya uwezo wa jumuiya.
- **Rasilimali:** mabadiliko ya rasilimali watu, vitu, na fedha.
- **Mazingira:** mabadiliko ya miundombinu ili iwe rafiki kwa watu wote.

Wakati Jumuiya za watu wenye ulemavu inawezekana zisiwe na ushawishi wa moja kwa moja katika mabadiliko ya kimfumo, kuna mambo mengi ambayo inawezekana tayari wanafanya ili kujenga uendelevu huo kama vile:

- Kujenga uwezo wa ushawishi katika ngazi ya jamii
- Kuwajengea uwezo watetezi na wanaharakati wa elimu mjumuisho
- Kushirikiana na skuli, serikali ya mtaa, na wadau wengine muhimu
- Kuisaidia kamati ya skuli ya elimu mjumuisho
- Kushirikiana na wazazi na familia za watoto wenye ulemavu

- Kutambua mali (na rasilimali) zilizopo katika jamii.
- Kujenga uelewa wa elimu mjumuisho na kusaidia kubadilisha mtazamo katika jamii.
- Shughuli za kiuchumi na kushirikiana na wafanyabiashara katika jamii ili kuchangisha fedha kwa ajili ya elimu mjumuisho.

Kipindi hiki kitazikumbusha jumuiya za watu wenye ulemavu kutafakari kuhusu shughuli ambazo tayari zimekuwa zikitekeleza kujenga uendelevu na kutokana na hizo kutambua 'mikakati mahususi' ya kuendeleza kazi ya utetezi katika elimu mjumuisho. Wataendelea kuainisha mikakati ipi waiimarishe zaidi na/au watekeleze zaidi katika Shehia zao na jinsi ya kutatua changamoto zinazokwaza uendelevu ambazo zinaweza kujitokeza.

### Katika kipindi hiki washiriki:

- ü Wataangalia mifano ya uendelevu katika elimu mjumuisho
- ü Kutafakari kuhusu mikakati ambayo tayari wamekua wakitekeleza kama jumuiya za Watu wenye ulemavu kwa ajili ya elimu mjumuisho
- ü Kuchunguza mikakati tofauti muhimu kwa ajili ya kuendeleza utetezi wa elimu mjumuisho
- ü Kujadili baadhi ya fursa na changamoto zinazozuia uendelevu katika mazingira yao.

## Shughuli nambari 4.1: Nini maana ya uendelevu?

1 dakika 45

### Maelekezo

- Adika neno **'uendelevu'** kwa herufi kubwa katikati ya karatasi ya chati mgeuzo.
- Waombe washiriki watumie dakika 2 – 3 kila mmoja akifikiri kuhusu neno hilo au vifungu vya maneno vinavyokuja katika akili yake anapofikiria neno 'uendelevu' na ayaandike kwenye karatasi. Unaweza kutoa mfano mmoja iwapo itasaidia.
- Baada ya dakika 2 – 3 waombe washiriki waseme baadhi ya maneno na vifungu vya maneno na viandike kwenye chati mgeuzo kuzunguka neno 'uendelevu' kwa mtindo wa ramani ya akili (au yabandike kama

ilivyooneshwa hapa chini). Chukua neno/kifungu cha maneneo kimoja pekee kutoka kwa mshiriki. Huhitaji kumuomba kila mtu.

- Waombe washiriki kuangalia maneno/vifungu vya maneno katika ramani ya akili (yasome tena kwa sauti kwa ajili ya wale wasioona) na waulize maswali yafuatayo:
  - **Umegundua nini katika maneno/vifungu vya maneno?**
  - **Kuna maudhui yoyote yanayofanana ambayo unayaona?**




- Jaribu kuchora **vipengele 4** vifuatavyo **vya uendelevu.** Waambie washiriki kwamba tunapofikiria uendelevu, tunaweza kufikiria kuhusu **mabadiliko ambayo yana athari ya muda mrefu** kwa kuhusisha maeneo manne yafuatayo. (Tafadhali kumbuka – hii ni namna moja tu ya kufikiria kuhusu/kuchambua uendelevu, lakini unaweza kufikiria vipengele vyengine vya kuzingatia).

### Ujumbe kwa mwezshaji

Kuna maneno na vifungu tofauti vya maneneo ambavyo washiriki wanaweza kuvifikiria watakapokua wanafikiria kuhusu 'uendelevu', na hivi si lazima vihusiane na elimu.

Labda washiriki wataanza kubaini kwamba maneno hayo yanaweza kuhusiana au kuingia katika zaidi ya vifungu/vipengele vilivyoelezwa hapa chini:

- Mfumo (sera na utekelezaji)
- Jamii (wazazi, mitazamo, muundo wa jamii)
- Jumuiya (uwezo, ushirikiano, mitandao, ujuzi, na elimu)
- Rasilimali (mgawanyo, bajeti, feedha, watu, vifaa)

Hata hivyo, usihofu iwapo maneno haya hayakutajwa. Kama mkufunzi, unaweza kupigia mstari au kuzungushia duara maneno ambayo yanahusiana na kipengele kimoja na ukaendelea kuelezea vipengele 4.

- Wasilisha kila nukta kwa kutoa mifano halisi kutoka katika jamii.

**Power Point** Kipindi cha 4 Slaidi ya 1: Vipengele vya uendelevu

**Mfumo wa elimu;** mabadiliko ya sera na utekelezaji. Kwa mfano sera jumuishi ya elimu ambayo imeidhinishwa katika ngazi ya skuli na inafahamika na kutumiwa na uongozi wa skuli. Serikali ya mtaa kutoka katika ngazi ya Shehia inashirikiana na jumuiya za watu wenye ulemavu kuhakikisha kwamba skuli za katika Shehia ni jumuishi. Hiyo ni ahadi ya kuhakikisha kwamba skuli zilizomo katika Shehia ni jumuishi.

**Jamii:** mabadiliko katika mifumo ya jamii na mabadiliko yanayoonesha kubadilika kwa mtazamo. Kwa mfano, vikundi vya wanajamii vimeanzishwa mfano wa kikundi cha wazazi wa watoto wenye ulemavu ambacho kinafanya kazi kama ni nyenzo na pia mfano wa kuigwa kwa familia nyengine.

**Jumuiya;** kubadilika kwa uwezo wa jumuiya. Kwa mfano, Jumuiya za watu wenye ulemavu ambazo zimepatiwa mafunzo ya kutetea elimu mjumuisho

na zina utaratibu wa kutathmini hatua wanazopiga kuelekea katika elimu mjumuisho.

**Rasilimali;** mabadiliko kwa rasilimali watu, vitu, na fedha. Kwa mfano, ushahidi wa elimu mjumuisho kujumuishwa katika bajeti za serikali ya mtaa na walimu kupatiwa mafunzo ya elimu mjumuisho.

- Waombe washiriki wakae katika vikundi vya watu 4 – 5. (Vyenginevyo, Shughuli hii inaweza kushirikisha washiriki wote katika kundi moja kama unadhani itakua vizuri zaidi).
- Katika vikundi vyao waombe washiriki wanakili jaduweli lililopo hapa chini kwenye chati mgeuzo na baadae wajadili swali lifuatalo kwa kila kipengele. Waandike mawazo yao kwenye chati mgeuzo. Toa mfano mmoja au miwili kwa kuwashirikisha iwapo itasaidia.

**Kuna mifano gani ya uendelevu kwa elimu mjumuisho kuhusiana na kipengele hiki?**

Power Point


### Kipindi cha 4: Maelekezo kwa ajili ya Shughuli

- Hakikisha kwamba washiriki wanafahamu kuwa si lazima mifano hii iwe ya mambo ambayo yameshafanywa katika mazingira yao bali ni orodha ya mambo ambayo ni vyema yangekuwepo ili kuhakikisha uendelevu.

| **Mfumo** | **Jamii** |
|---|---|
| **Shirika/Jumuiya** | **Rasilimali** |

- Kama muda utaruhusu, viombe vikundi viwili kujumuika kubadilishana na kulinganisha mawazo yao kabla hawajaingia katika majadiliano.
- Katika majadiliano viite vikundi tofauti kwa zamu ili waeleze mifano yao na iandike kwenye chati mgeuzo. Hakikisha kwamba kila kikundi kinachowasilisha kinaongeza wazo jipya katika orodha. Aidha yaandike mawazo haya katika chati mgeuzo moja kama ilivyooneshwa hapa chini au kwenye karatasi tofauti za chati mgeuzo ukihitaji nafasi zaidi. Zibandike

katika kuta za ukumbi ili kuzirejea baadae katika Shughuli nambari linalofuata.




**Note to facilitator**

Below are some of the examples of sustainability in relation to inclusive education for each of the components, but this is not an exhaustive list and participants may come up with additional ideas of their own

| **System** | **Community** |
|---|---|
| Inclusive education framework and policies in place at national level and policies in place and understood at local level.<br><br>Teachers trained and using inclusive education practices in the classroom.<br><br>Schools' environment adapted | Parents and caregivers understand the importance of education for their children.<br><br>There is community ownership and contribution towards making schools more inclusive.<br><br>School inclusion teams have been set up involving wider members of the community |

| Organisation | Resources |
|---|---|
| The OPDs function well and have identified personnel to lead on inclusive education advocacy.<br><br>The OPDs incorporate inclusive education into their strategic planning processes | There is evidence of innovative use of local resources for addressing barriers to inclusive education.<br><br>There is collaboration and networking across the community to identify resources |

## Shughuli nambari 4.2: Mikakati ya kuendeleza kazi ya utetezi katika elimu mjumuisho.

1 dakika 90

### Maelekezo

- Waombe washiriki waunde vikundi vya watu 4 – 5. Kila kikundi kiteuwe mwenyekiti, katibu, mtunza muda na muwasilishaji.
- Waombe washiriki katika vikundi wajadili maswali yafuatayo na katibu aandike majibu yao kwenye chati mgeuzo:

**Kama jumuiya za watu wenye ulemavu, tafadhali tafakarini yafuatayo:**

§ **Mambo gani ambayo tayari mmekuwa mkiyafanya kujenga na kuimarisha elimu mjumuisho?**

§ **Kwa nini jambo hilo ni muhimu kwa ajili ya uendelevu?**

**Power Point**

**Kipindi cha 4: Slaidi ya 1: Mikakati ya kuendeleza kazi ya utetezi katika elimu mjumuisho.**

- Kusaidia mjadala wa swali waombe washiriki kujikumbusha vipengele tofauti vya uendelevu walivyovijadili- kwa kina siku iliopita (mf. mfumo, jamii, jumuiya, na rasilimali). Vikundi viwe makini sio tu kutaja shughuli walizofanya (mf. kuandaa kipindi cha redio kuhusu elimu mjumuisho), lakini hatua ambazo zilisaidia uendelevu (mf. jumuiya imeandaa shughuli za kukuza uelewa mwaka ujao na imezijumuisha katika mpango mkakati wao).
- Mwenyekiti wa kila kikundi ahakikishe kwamba kila mwanakikundi anachangia katika mjadala.

- Baada ya kujadiliana kwa dakika 20. Waambie washiriki kwamba sasa tutaangalia mikakati mahususi ya kusaidia uendelevu. Gawa kwa kila kikundi seti ya **mikakati ya uendelevu** iliokatwa katika vipande vya karatasi.
- **Nyenzo 4.2: Mikakati muhimu ya kuendeleza kazi ya utetezi katika elimu mjumuisho.**

**Nyenzo nam.4.2**

**Mikakati muhimu ya kuendeleza kazi ya utetezi wa elimu mjumuisho.**

- Orodha za 'mikakati ya uendelevu' imeandikwa hapa chini. Hii sio orodha yote, na washiriki wanaweza kuwa na nyorodha nyengine ambazo wangependa waongezee. Baadhi ya mikakati kama vile 'kuendesha kampeni ya utetezi katika ngazi ya taifa' inahitaji usaidizi maalumu wa ziada na muongozo lakini inajumuishwa kama mfano wa mkakati wa utetezi. **Unaweza pia kuamua kuondoa baadhi ya mikakati ukihisi imekua mingi mno.**

- Kujenga uwezo wa utetezi katika ngazi ya mtaa (mf. kuwapatia mafunzo viongozi wa jumuiya za watu wenye ulemavu)
- Kuwapatia mafunzo watetezi jamii na wanaharakati wa elimu mjumuisho
- Kushirikiana na skuli, serikali ya mtaa, na wadau wengine muhimu
- Kuwatambua na kushirikiana na watu mashuhuri katika ngazi ya jamii (mf. viongozi wa dini, Mwenyekiti wa Baraza la Mtaa)
- Kushirikiana na Kamati ya Skuli ya Elimu mjumuisho
- Kushirikiana na serikali ya mtaa
- Kushirikiana na wazazi na familia za watoto wenye ulemavu
- Kuanzisha vikundi vya ushirikiano katika ngazi ya mtaa kama vile vikundi vya wazazi vya kusaidiana
- Kutambua rasilimali (na nyenzo) zinazopatikana ndani ya jamii
- Kujenga uelewa wa elimu mjumuisho na kusaidia kupambana na mitazamo hasi katika jamii.
- Kutumia sera kushawishi mabadiliko.
- Kuendesha kampeni za kitaifa za utetezi
- **Kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli na kuwapatia vifaa saidizi**
- **Shughuli za kiuchumi/kushirikiana na wafanyabiashara au wahisani,** kuchangisha fedha kwa ajili ya elimu mjumuisho
- Kuendelea **kutafakari walichojifunza** na kutumia ujuzi huo **kurekebisha mipango ya utetezi.**


| | |
|---|---|
| **Mfumo** | **Jamii** |
| **Jumuiya** | **Rasilimali** |

- Waombe washiriki katika kila kikundi kujikumbusha jaduweli la 'vipengele 4 vya uendelevu'.
- Baadae waombe washiriki katika vikundi vyao kujaribu kubandika mikakati katika moja kati ya vifungu vinne vya maswali:
    - **Mkakati huo unasaidia eneo gani la uendelevu?**
- Weka bayana kuwa kutakuwa na mpishano na baadhi ya mikakati itasaidia zaidi ya eneo moja la uendelevu. Kwa mfano, '**Kushirikiana na kamati ya elimu mjumuisho ya skuli'** kunasadifu pia katika kifungu cha **'mfumo'** na **'jamii'.**



Wanachama wa Jumuiya za watu wenye ulemavu kutoka Zanzibar wakijadili mikakati tofauti iliyoandikwa kwenye karatasi.

[Maelezo ya picha: Picha inaonesha watu tisa (wanawake wanne na wanaume watano) wakihudhuria warsha, wanafanya kazi katika kikundi, wakiangalia chati mgeuzo wakati mshiriki mmoja anaandika, na mshiriki mwengine anasoma kwa sauti]




Mfano wa mikakati tofauti iliobandikwa kwenye chati mgeuzo chini ya vichwa vinne vya habari ambavyo ni: mfumo, jamii, jumuiya, na rasilimali.

[Maelezo ya picha: Picha inaonesha kadi kubwa ya buluu iliogawanywa katika vyumba vinne, kila chumba kina kichwa kimoja cha habari: mfumo, jamii, jumuiya, na rasilimali. Kuna vipande vya karatasi nyeupe vyenye maandishi vilivyobandikwa chini ya kila kichwa cha habari]

**Ujumbe kwa mkufunzi**

Tunaitofautisha mikakati kama hivi ili kusaidia kutambua wapi kuna upungufu na wapi tuelekeze nguvu zaidi ili kujenga uelewa.
Katika ukurasa mwengine kuna mfano wa kifungu na mkakati unaonasibiana nacho. Hii SIO namna pekee ya kupangilia mikakati. Vikundi vijadili na kueleza KWA NINI wanafikiri mkakati maalumu hunasibiana na kifungu fulani.

Pia kuna karatasi za ziada ambazo hazijaandikwa ili kuviwezesha vikundi kuongeza mikakati ya ziada ambayo wanadhani inapaswa kujumuishwa.

- Hatimae, washiriki katika vikundi vyao waoneshe mfano mmoja kutoka katika orodha ya shughuli ambazo wamekua wakizifanya kama jumuiya za watu wenye ulemavu ambazo walijadiliana mwanzo wa Shughuli, ambazo zinasadifu mkakati.

- Katika majadiliano pitieni kila mkakati na viombe vikundi tofauti kueleza:
    - Wameweka kifungu kipi na kwa nini
    - Mfano wa shughuli ambayo inasadifu mkakati.
- Kumbuka: Rasilimali zipelekwe pale penye changamoto zaidi.  Pia ni muhimu kutambua kuwa msaada ni muhimu kuelekezwa katika maeneo yenye rasilimali chache na kuangalia jinsi gani ya kuendelea kutafuta fursa zaidi kwa ajili ya  msaada zaidi wa  fedha.

Mfano wa jinsi gani mikakati inaweza kuorodheshwa katika kila kifungu – lakini inaweza pia kuwekwa katika mpangilio tofauti iwapo mshiriki ataweza kueleza kwa nini anadhani mkakati huo uwekwe katika kifungu fulani.

| **Mfumo** | **Jamii** |
|---|---|
| – Kushirikiana na kamati ya elimu mjumuisho ya skuli<br>– Kushirikiana na serikali ya mtaa<br>– Kutumia sera kushawishi mabadiliko<br>– Kuendesha kampeni ya kitaifa ya utetezi | – Kushirikiana na skuli, serikali ya mtaa, na wadau wengine<br>– Kutambua na kushirikiana na watu mashuhuri katika jamii<br>– Kushirikiana na wazazi na familia za watoto wenye ulemavu<br>– Kuanzisha vikundi vya ushirikiano katika jamii kama vile vikundi vya wazazi vya kusaidiana<br>– Kukuza uelewa wa elimu mjumuisho na kusaidia kuondokana na mitazamo hasi katika jamii |
| **Jumuiya** | **Nyenzo** |
| – Kujenga uwezo wa utetezi katika ngazi ya jamii (mf. kuendesha mafunzo kwa viongozi wa jumuiya za watu wenye ulemavu)<br>– Kuendesha mafunzo kwa watetezi jamii na wanaharakati wa elimu mjumuisho<br>– Kuendelea kutafakari kuhusu ulichojifunza na jinsi ya kutumia ujuzi huo kurekebisha mipango ya utetezi.<br>– Kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli na kutoa vifaa saidizi | – Shughuli za kiuchumi/kushirikiana na wafanyabiashara kuchangisha fedha kwa ajili ya elimu mjumuisho.<br>– Kutambua rasilimali (na nyenzo) zinazopatikana katika jamii. |

**Muendelezo wa zoezi: lenga katika mkakati wa 'Kushirikiana na wazazi'**

Kama muda unaruhusu, tumia muda kuangazia mkakati wa 'kushirikiana na wazazi.

- Sisitiza nukta ya kwamba wakati wadau wengine wanakuja na kuondoka, wazazi siku zote wapo na kwa sababu hiyo ni muhimu kwa ajili ya uendelevu. Kwa hivyo ni muhimu kwetu kuzingatia ni jinsi gani tunaweza kuendelea kushirikiana na kuwasaidia wazazi.
- Waombe washiriki kutoa mifano tofauti ya jinsi gani wanaweza kushirikiana na wazazi (mifano hii inaweza kuwa ilishatajwa hapo nyuma).
- Iandike kwenye chati mgeuzo. Mifano inaweza kujumuisha ifuatayo lakini hakikisha unaongeza mifano ya washiriki pia:
  - kuwasaidia wazazi kuhudumia watoto wao nyumbani
  - Kutoa msaada wa mafunzo endelevu kwa wazazi kulingana na mahitaji
  - kutambua wazazi wa watoto wenye ulemavu ambao ni 'mifano ya kuigwa' kama ni mabalozi wa Elimu mjumuisho
  - kuanzisha vyama/vikundi vya kusaidiana vya wazazi wa watoto wenye ulemavu
  - kuziunganisha familia na huduma za marekebisho
- Kuonesha picha /video za wazazi/walezi zikionesha jinsi wanavyojishughulisha na walivyoathiriwa na kazi ya utetezi wa elimu mjumuisho inayofanywa na JWU.
- Karibisha maswali na majadiliano.

## Shughuli nambari 2.3: Kuimarisha uendelevu kwa ajili ya utetezi wa elimu mjumuisho

Katika Shughuli ifuatayo washiriki watafakari kila mkakati na kuzingatia fursa zilizopo katika kuimarisha uendelevu wa elimu mjumuisho katika Shehia au jamii zao. Shughuli hii inaweza kuhitaji kufanyika baada ya mapumziko ya chakula cha mchana.

1 dakika 45

### Maelekezo

Wakiwa katika vikundi vile vile, waombe washiriki watafakari **mikakati ya uendelevu wa elimu mjumuisho** na kufikiria maeneo ambayo yana fursa kwao kuimarisha uendelevu katika elimu mjumuisho. Walenge zaidi katika yale maeneo ya mkakati ambayo kwa sasa hayajafanikiwa sana/ hawana mifano kutoka katika harakati zao za karibuni za utetezi.

**Power Point** **Kipindi cha 4 PPT: Slaidi ya 3: Kuimarisha uendelevu kwa ajili ya utetezi wa elimu mjumuisho.**

- Vikundi vijadili maswali:
  - **Mikakati ipi tunaweza kuitekeleza vizuri zaidi?**
  - **Tutumie zaidi mikakati ipi?**
  - **Orodhesha mapendekezo/hatua za kuchukua ili kuimarisha uendelevu kwa** kulinganisha mikakati unayotaka kuilenga.
- Unaweza pia kupitia bango la mafanikio la siku iliyopita na orodha ya shughuli ambazo wanazifanya sasa hivi.
- Vikundi vichague mikakati wanayotaka kuilenga na **viorodheshe mapendekezo madhubuti ya uendelevu/hatua kuhusiana na mkakati huo.** Waandike mkakati kwa rangi moja juu ya karatasi na mapendekezo/hatua chini yake kwa rangi tofauti. Wakati wa majadiliano watake washiriki katika vikundi vyao kuelezea mapendekezo na hatua na ziandike kwenye chati mgeuzo. Hakikisha kwamba hakuna nukta inayoandikwa zaidi ya mara moja. Kama muda unaruhusu, washiriki wote kwa pamoja wajaribu kutambua ni mapendekezo na hatua gani ni vipaumbele na yapigie mstari kwa rangi tofauti.

## Kipindi cha 4.4: Kutatua changamoto za uendelevu – igizo dhima shirikishi.

1 dakika 150 (dakika 30 za maandalizi na saa 2 kwa ajili ya maigizo-dhima shirikishi)

### Maelekezo

- Fanya Shughuli ya kuchekesha ili kuwapanga washiriki katika vikundi vipya. Kuwe na vikundi vingi kulingana na nafasi za kuigiza katika igizo hilo. (vikundi visizidi 6 kwa jumla).
- Waombe washiriki kuangalia tena orodha ya mapendekezo/hatua ambazo zilipendekezwa katika Shughuli iliyopita.
- washiriki katika vikundi vyao wajadili changamoto zozote zinazoweza kujitokeza au katika utekelezaji wa kila hatua.
- Katika majadiliano pokea mrejesho na andika changamoto katika karatasi tofauti, ukihusisha changamoto na mapendekezo/hatua.
- Baadae wapatie kila kikundi **'kisa (hali) kutoka katika Nyenzo 4.3** ambayo inaelezea changamoto fulani ya uendelevu kwa kina.

**Nyenzo nambari 4.3**

**Slaidi ya 4: Hali ya igizo inayoelezea changamoto za uendelevu katika elimu mjumuisho**

**Power Point**

**Kipindi cha 4 PPT: Slaidi ya 4: Kuandaa igizodhima lako**

- Muombe mshiriki mmoja katika kikundi kusoma kwa sauti hali ya igizo kwa umakini. Baadae wajadili kama kikundi watafanya vipi igizo dhima lao. Kama sehemu ya maandalizi yao, wajadili yafuatayo:
  - Hali ikoje na kuna changamoto gani?
  - Nani watakao husika? (katika kikundi chenu nani ataigiza nafasi gani?)
  - Vipi unaweza kwa ufasaha kuonesha hali halisi na changamoto kwa hadhira?
  - Taarifa zipi unaweza kuongeza katika igizo ili liakisi uhalisia?

- Waambie washiriki kuwa wana dakika 15 – 20 za kujiandaa kwa igizo lao. Kila mmoja katika kikundi ahusike. Iwapo mwanakikundi hataki kuigiza, anaweza kusaidia kutoa muongozo/kuandaa igizo.
- Wakumbushe washiriki kuwa hawajaribu kutatua changamoto kupitia igizo bali ni kuonesha tatizo lenyewe tu.
- Vikundi vitakapokuwa tayari, vikaribishe kuonesha igizo lao kikundi kimoja baada ya chengine. Baada ya kila kikundi kuigiza, waombe waendelee kubaki mbele, waulize watazamaji maswali yafuatayo au yanayofanana na haya:
    - Nini ilikuwa changamoto? Nani alihusika? Kipi kilikua chanzo cha tatizo?
    - Uliweza kutambua changamoto? Umewahi kukutana na changamoto kama hizo katika mazingira yako?
    - Ungefanya nini katika hali kama hii? Utatatua vipi changamoto hii? Kuna mtu mwengine yeyote anayehitajika kutatua changamoto hii?
- Kufikia hapa, iwapo mshiriki kutoka miongoni mwa hadhira atatoa suluhisho la maana, muite aje ‘kuonesha’ suluhisho hilo kwa kuigiza na kikundi kilichomaliza kuigiza. Hii itakuwa ni kuboresha na umuite mshiriki aje kuigiza iwapo tu ataonesha kujiamini na yupo tayari kufanya hivyo.
- Ruhusu hatua hiyo kuendelea kwa dakika chache au mpaka pale mkakati kwa ajili ya kutatua tatizo hilo utakapokuwa umeoneshwa. Baadae uliza maswali yafuatayo:
  - **Je, Imeakisi uhalisia? Inaweza kutokea kweli?**
  - **Kuna mtu mwengine mwenye mawazo tofauti?**
- Unataka kutathmini katika hatua hii iwapo washiriki wanaeleza mikakati muafaka kwa ajili ya kutatua changamoto ambayo inaweza kutumika katika maisha halisi.
- Endelea na mchakato huo huo kwa vikundi vyengine (au fanya kulingana na muda ulionao). Hatua kuu ni:

1. Igizo la kuonesha changamoto.
2. Mkufunzi anauliza maswali kuhusu hali kutathmini ufahamu.
3. Mkufunzi anakaribisha ushauri/mikakati.
4. Hadhira ‘wanaigiza’ mikakati na waigizaji.
5. Mkufunzi anauliza maswali baada ya washiriki kueleza mikakati.

## Ujumbe kwa mkufunzi

Mbinu zilizoelezwa hapo juu kwa ajili ya kuhamasisha ushiriki wa hadhira zimeigwa kutoka katika ‘Jukwaa la maigizo’, aina ya igizo shirikishi lililoasisiwa na raia wa Brazil Augusto Boal.

Dhamira ya mkufunzi ni kusaidia kuandaa mazungumzo na jamii (hadhira) baada ya igizo kumalizika katika nukta ya changamoto au ‘mgogoro’. Waigizaji watabakia mbele na mkufunzi atakuja mbele na kuanza kuuliza maswali. Ahakikishe hadhira inamsikiliza na imechangamka, vyenginevyo hadhira inaweza kupoteza hamu ya kushiriki.

Dhamira kuu ya mazungumzo ni kuelezea mikakati tofauti na mingi kadiri inavyowezekana kutatua matatizo yaliyowasilishwa. Ni chombo cha majadiliano ya pamoja cha kutatulia changamoto. Ambapo jamii (hadhira) inamiliki changamoto na utatuzi wake.

Hapa chini kuna maswali ambayo unaweza kuuliza. Huhitaji kuuliza maswali yote au katika mpangilio huu; ni mapendekezo tu lakini, mara zote ni lazima uulize maswali na SIO kujibu wewe mwenyewe.

<u>Mkufunzi anauliza maswali kuhusu changamoto</u>

- Uliona nini katika igizo?
- Kilitokea nini?
- Kulikuwa na matatizo yoyote katika igizo? Ni yepi hayo?
- Unaitambua hali hii?
- Je, Hii inatokea katika jamii yako?
- Wangapi katika washiriki hapa wamewahi kukumbwa na tatizo hili? (au wanamjua mtu ambaye amewahi kukabiliwa na tatizo hili)? (nyoosha mkono!)

<u>Mkufunzi akikaribisha mapendekezo/mikakti</u>

- Ungefanyaje katika hali hii?
- Mtu (anaekabiliwa na tatizo) afanye nini?
- Kuna ushauri wowote mwengine?
- (Baada ya kupokea ushauri), mnakubaliana nae?

<u>Hadhira ‘inaigiza’ mikakati na waigizaji wengine</u>

- Waombe watu mbalimbali miongoni mwa hadhira kutoa mawazo yao – akijitokeza mtu mwenye wazo zuri mkaribishe mbele aje kuigiza.

- Waombe waigizaji mahususi waje mbele na wabuni igizo pamoja na hadhira ‘akijaribu’ kuigiza wazo lake.

Mkufunzi akiuliza maswali baada ya hadhira kueleza mikakati:

- Ishukuru hadhira na watake wapige makofi.
- Uliza: Unafikiri nini kuhusu ulichokiona?
- Unalionaje wazo hili?
- Unakubaliana na alichokifanya?
- Kina uhalisia?
- Kuna yeyote mwenye wazo jengine?

Endelea kuwakaribisha watu zaidi iwapo wana ushauri wa kuwaeleza washiriki. Lengo ni kupata mikakati tofauti; hakuna jibu sahihi au lisilo sahihi! Hakuna haja ya kukubaliana na mkakati mmoja tu kwa kuwa kunaweza kuwepo namna tofauti za kutatua changamoto.

Mwisho, washukuru wote kwa michango yao kabla ya kuanza igizo jengine.

Moduli ya

# 4

# Vielelezo na vitini


## Nyenzo nambari 1.1: Kadi za mapitio ya elimu mjumuisho

## 1.1a Uwepo, Ushiriki, Mafanikio

**Uwepo** kupata na kuhudhuria shule



**Ushiriki** kujiunga na shughuli za kimasomo na kijamii




**Mafanikio** kufikia ukomo wa uwezo wao

[Maelezo ya picha 1: Sehemu ya mbele ya picha kuna watoto wawili wa kike, mmoja akiwa na ulemavu wa ngozi, wamekaa sakafuni wanacheka wakiwa na karatasi kubwa kati yao yenye maandishi na michoro. Sehemu ya nyuma kuna watoto wawili wa kiume, mmoja akiwa na gongo la kutembelea, wanabandika bango kubwa ukutani. Upande wa kulia kuna watoto watatu wamekaa wakielekeana kwenye dawati, watoto wawili wa kike na mmoja wa kiume na mwalimu ametabasamu na amewainamia. Wote wapo darasani wakiwa na karatasi zenye maandishi ukutani]

[Maelezo ya picha 2: Watoto watatu wa kike wanacheza nje, jengo la skuli likionekana nyuma yao. Mtoto mmoja wa kike akiwa kwenye kitimwendo ameshikilia ncha moja ya kamba na mwengine ameshikilia ncha ya pili. Wote wamevaa sare za buluu na hijabu nyeupe. Mtoto wa tatu wa kike aliyevaa sare ya buluu na hijabu nyeupe anaruka kamba. Wote wanatabasamu.]

# 1.1b: Aina 6 za vikwazo vya elimu elimu mjumisho

**1. Vikwazo vya kimazingira:** kwa mfano, madarasa yasiofikika



**2. Vikwazo vya kimtazamo:** kwa mfano wazazi wasiothamini elimu




**3. Vikwazo vya kisera:** kwa mfano, hakuna sera inayoruhusu wanafunzi waliojifungua kurudi skuli





**4. Vikwazo vya kiutendaji:** mf. walimu hawatumii mbinu jumuishi za kufundundishia



**5. Vikwazo vya taarifa:** kwa mfano, wazazi hawajui kuwa mtoto wao anaweza kwenda skuli



**6. Vikwazo vya rasilimali:** kwa mfano, ukosefu wa walimu wenye ujuzi na madarasa



[Maelezo ya picha 1 (vikwazo vya kimazingira): mtoto wa kiume amekaa kwenye kiti mwendo anaangalia chini. Kuna ngazi ndefu nyuma yake ya kupanda ili afike darasani. Kupitia mlangoni anaonekana mwalimu anasomesha.]

[Maelezo ya picha 2 (vikwazo vya kimtazamo): Mtu mzima mwanamme amekaa mbele ya zuma lililowekwa juu ya meza. Mtoto mdogo wa kiume akiwa amevaa sare ya skuli ameshika karatasi zenye maandishi akimuonesha yule mtu aliyekaa. Yule mtu anaangalia upande mwengine mikono yake ikiwa ameinyoosha juu. Sura yake inaonesha amekasirika.]


[Maelezo ya picha 3 (vikwazo vya kisera): Sehemu ya mbele ya picha inamuonesha mtoto wa kike akiwa amevaa sare ya skuli na anaonekana ni mja mzito. Anaangalia chini. Mtu mzima mwanamme aliyevaa shati na tai amesimama akimuashiria atoke nje ya skuli. Kwa mbali upande wa nyuma wa picha kuna watoto watatu waliovaa sare za skuli ambao wapo pembeni ya jengo la skuli.]

[Maelezo ya picha 4 (vikwazo vya kiutendaji): Mwanamke mtu mzima amesimama mbele ya wanafunzi ambao wamekaa kwenye madawati. Anaashiria juu na anazungumza akiwa kawaelekezea mgongo. Mbele ya darasa kuna mwanafunzi mmoja anaangalia nje kupitia dirishani na mwanafunzi mwengine amelaza kichwa chake kwenye mikono yake juu ya dawati.]

[Maelezo ya picha 5 (vikwazo vya taarifa): Kuna picha mbili zilizotenganishwa na mstari mrefu wa rangi nyekundu. Picha ya upande wa kushoto inaonesha jengo linalosomeka SERA ZA ELIMU ubavuni. Jengo hilo lipo nyuma ya uzio wa waya. Kupitia dirishani kunaonekana marundo ya karatasi zilizoparaganyika. Picha ya upande wa kulia inamuonesha mtu mzima mwanamme na mwanamke wakiwa nje ya nyumba ilioezekwa nyasi. Wamenyoosha mikono yao juu ikiashiria hawafahamu. Nje ya nyumba kwenye mkeka kuna mtoto mwenye mguu mmoja aliyelala].

[Maelezo ya picha 6 (vikwazo vya rasilimali): Darasa lenye idadi kubwa ya wanafunzi wakiwa wamekaa kwakubanana kwenye safu. Mwalimu anaonekana kwa mbali mbele ya darasa akiashiria aandishi ubaoni. Kuta na madirisha ya darasa zimechakaa.]

## 1.1c: Vipengele vya mfumo wa elimu mjumuisho



[Maelezo ya picha: Picha katika ukurasa uliopita inaonesha mifano kumi ya vipengele tofauti vya mfumo wa elimu kwa maandishi na picha za michoro. Kuelekea kulia kuanzia juu mfano wa kwanza ni 'takwimu za elimu'. Picha ilioambatana nayo ni kiwambo cha kompyuta na baobonye kando ya rundo la karatasi zenye maandishi. Mfano wa pili ni wasimamizi wa elimu na maafisa. Picha ilioambatana nayo ni vitabu vikubwa sana vilivyopandishiwa kimoja baada ya chengine na mtu aliyevaa tai nyuma yake akiwa juu kama aliyekaa nyuma ya meza. Mfano wa tatu ni wanafunzi. Picha iliyoambatana nayo ni kikundi cha wanafunzi watano na vijana wa kuchora akiwemo mwanamke na mwanamme, mtu mmoja aliyevaa miwani myeusi ameshika fimbo na mtu mwengine ameshika gongo la kutembelea na mtu mwengine mwanamke amevaa hijabu. Mfano wa nne ni 'mitihani na tathmini'. Picha inayoambatana nayo ni ya mchoro wa mtu aliyekaa mezani akiwa ameshika kalamu juu ya karatasi anaangalia chini. Kuna saa ukutani nyuma yake. Mfano wa tano ni 'bajeti na fedha'. Picha iliyoambatana nayo ni ya mabunda mawili ya pesa yakiwa na alama ya dola za Marekani juu yake. Mfano wa sita ni skuli na taasisi za elimu'. Na picha iliyoambatana nayo ni jengo la ghorofa tatu lenye madirisha mengi na alama inayosomeka 'Chuo Kikuu' upande wa kushoto na majengo mawili ya chini yalioezekwa kwa mabati, yakiwa na maandishi yanayosomeka 'skuli' upande wa kulia. Mfano wa saba ni 'Sheria na sera'. Picha iliyoambatana nayo ni marundo mawili ya karatasi. Moja likiwa na maandishi yanayosomeka 'SHERIA' juu yake na jengine likisomeka 'SERA' juu yake. Mfano wa saba ni 'walimu na maafisa mafunzo'. Picha iliyoambatana nayo ni ya mchoro wa mwanamke aliyeshika fimbo ndefu akionesha kwenye ubao wenye maandishi. Mfano wa tisa ni wa 'wazazi na wanajamii'. Picha iliyoambatana nayo ni ya kikundi cha watu saba wa kuchora akiwemo mwanamke aliyemshika mkono mtoto, mwanamke aliyekaa kwenye kitimwendo, mtu mrefu mwembamba aliyevaa tai, na mwengine mfupi mnene, mwanamke wa tatu na kikongwe anaetembelea fimbo. Picha ya kumi ni vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Picha iliyoambatana nayo ni ya vitabu vitatu kimoja kikiwa kikubwa kuliko vyengine na kimoja kilichofumwa kwa spiringi, rula, penseli, kalamu na kifutio.]

### 1.1d: Vikwazo vyenye uhusiano katika elimu mjumuisho



Upungufu wa walimu waliopata mafunzo vizuri



Walimu wachache wenye mafunzo duni na darasa kubwa



Walimu wachache wenye mafunzo duni na darasa kubwa



Wanafunzi wanatoroka skuli na kufanya kazi ya kusafisha na kuuza samaki



Wazazi au walezi hawaoni umuhimu wa kupeleka watoto wao skuli.




Skuli ipo mbali na makaazi ya wanafunzi

[Maelezo ya picha: Kuna picha sita tofauti zilizounganishwa pamoja kwa mishale. Picha ya kwanza inaonesha mnchoro wa mtu unaowakilisha mwanamke, ambae ameshika fimbo akionesha kwenye ubao ambao una maandishi. Kuna duara kubwa la rangi nyekundu na mstari mwekundu uliopita katikati ya mchoro huu wa mtu. Chini ya picha 1 kuna maneno yanayosomeka, 'upungufu wa walimu waliopatiwa mafunzo sahihi'. Kuna mshale unaounganisha picha hii na picha nyengine inayoonesha darasa lililosheheni wanafunzi huku wanafunzi wengi wakiwa wamebanana wakikaa katika mtindo wa safu. Mwalimu anaonekana kwa mbali mbele ya darasa akiashiria kwenye ubao wenye maandishi. Kuta za darasa na madirisha yamechakaa. Chini ya picha 2 kuna maandishi yanayosomeka, 'walimu wachache waliopatiwa mafunzo hafifu wakiwa na madarasa yaliosheheni wanafunzi'. Mshale unaunganisha picha hii na picha ya tatu inayomuonesha mwanamke aliyesimama mbele ya wanafunzi waliokaa katika madawati. Anaashiria juu huku akizungumza. Amewaelekezea mgongo. Mbele ya darasa kuna mwanafunzi ambae anaangalia nje kupitia dirishani na mwengine amelaza kichwa chake kwenye mikono juu ya dawati. Chini ya picha 3 kuna maandishi yanayosomeka, 'wanafunzi wanasoma elimu duni'. Mshale unaunganisha picha hii na picha 4 ambayo inawaonesha wanafunzi watatu wakiwa wameshika karatasi. Wawili kati yao wametabasamu na kuna maandishi 90% na 100% yanayoonekana katika karatasi zao. Mwanafunzi wa tatu amehuzunika na amejitenga mbali kidogo huku karatasi yake ikiwa na maandishi 20%. Chini ya picha 4 kuna maandishi yanayosomeka, 'wanafunzi wanaoamua kuacha skuli kwa sababu hawasomi'. Kuna mshale unaounganisha picha hii na picha 5 inayomuonesha mtu aliyekaa mbele ya zunma lililowekwa juu ya meza. Mtoto wa kiume aliyevaa sare za skuli ameshika karatasi zenye maandishi akimuonesha yule mtu. Yule mtu anaangalia upande mwengine huku akinyoosha mikono yake juu. Sura yake inaonesha amekasirika. Neno 'na' linaunganisha picha ya tano na picha ya sita na picha ya mwisho inayoonesha njia ndefu ya watembea kwa miguu ambayo inaelekea vilimani na inakatisha kwenye michirizi miwili au mito na madaraja madogo ya mbao. Kwa mbali upande wa kulia kuna Kijiji. Watoto wawili waliovaa sare za skuli wanatembea katika njia hiyo. Chini ya picha 6 kuna maandishi yanayosomeka, 'skuli ipo mbali sana na makaazi ya wanafunzi'.]

## 1.1e: Duara (Mzunguko) wa ubaguzi

**Mzunguko wa ubaguzi**

Watoto wa kiume wanapelekwa skuli.



Mtaala wa masomo unahamasisha ubaguzi wa jinsia.






Mama vijana wanatengwa shuleni kutokana na sera na mazoea.

Duara hasi la ubaguzi linaendelea.




[Maelezo ya picha: kuna mchoro wenye picha nne na kila picha imehusishwa na picha nyengine kwa mshale. Maneno ‘duara la ubaguzi’ yameandikwa katikati. Picha iliopo juu ya mchoro inamuonesha mtoto mdogo wa kike akisafisha sakafu ya chumba na ndoo ikiwa pembeni yake. Kuna sofa nyuma yake na picha mbili zilizotundikwa ukutani, moja ikiowaonesha watu wanne (watu wazima wawili na watoto wawili) na nyengine ikiwaonesha watoto wawili. Mtoto wa kiume anapita kando ya mtoto wa kike ambae anasafisha sakafu. Amevaa sare ya skuli na kabeba begi la skuli mgongoni. Yule mtoto wa kike anamuangalia. Anaonekana mwenye huzuni. Picha iliopo upande wa kulia wa mchoro inawaonesha watoto wanne wakiwa wamekaa darasani. Watoto wawili wa kike wamekaa pamoja na wanaangalia picha katika kitabu. Picha inamuonesha mwanamke anapika na mwanamme aliyevaa tai ameshika begi la ofisini. Sura ya mtoto wa kike inaonesha hali ya kuchanganyikiwa au mshangao. Picha iliopo chini ya mchoro inamuonesha mtoto wa kike aliye katika rika la baleghe (mwari) ambae hajavaa sare ya skuli, akiwa amembeba mtoto mgongoni. Amesimama nje ya jengo la skuli akiangalia ndani. Anaonekana mwenye huzuni. Kuna watoto wawili wa kike waliovaa sare za skuli ambao wamesimama mbele ya skuli wanamuangalia huku wakizungumza. Picha iliopo upande wa kushoto wa mchoro inamuonesha mwanamke aliyekaa juu ya kigoda akichambua mboga na kuzitumbukiza kwenye chungu. Kando yake kuna mtoto wa kike aliyekaa juu ya kigoda, nae pia anachambua mboga. Sura ya mtoto wa kike inaonesha si mwenye furaha. Sura ya yule mwanamke inaonesha ni mwenye kukata tamaa au ana hofu. Wapo kimya. Kuna sufuria ya kupikia iliopo chini kando yao.]

## 1.1f: Ushirikiano endelevu na kamati ya elimu mjumuisho ya skuli




[Maelezo ya picha: Kuna watu wanane waliokaa nje chini ya mti katika muundo wa nusu duara. Wamekaa kwenye viti. Nyuma yao kuna skuli, baadhi ya watoto wanacheza nje ya skuli. Kuna wanawake watatu katika kikundi hicho. Kuna mtu aliyekaa kwenye kitimwendo na mwanamme kikongwe akiwa na gongo la kutembelea. Kuna mtu kwenye kikundi ambae anaonesha ishara kwa mikono yake. Mwanamke mmoja anazungumza na kuashiria. Pembeni yake kuna gongo la kutembelea lililowekwa chini.]


**1.1g: Mratibu wa Elimu mjumuisho, kupitia kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ya, anaweza kusaidia uratibu katika ngazi tofauti.**



Jamii






Maelezo ya picha: Kuna mtu aliyekatwa mguu mmoja, akiwa amesimama na ameelekea mbele, ametabasamu, mkono wake mmoja akiwa ameshikilia gongo la kutembelea na mkono mwengine akiashiria. Upande wa juu kushoto kuna mchoro wa watu nane akiwemo mwanamke aliyemshika mkono mtoto, mwanamke aliyekaa kwenye kitimwendo, mwanamme mrefu mwembamba aliyevaa tai na mwanamme mfupi mnene, mwanamke mwengine wa tatu na mtu mwengine kikongwe anaetembea kwa gongo la kutembelea na neno ‘jamii’ limeandikwa chini yake. Sehemu ya chini kushoto kuna jengo kubwa la serikali likiwa na rundo la karatasi mbele yake na neno ‘sera’ limeandikwa juu yake. Kwa upande wa kulia kuna jengo la skuli likiwa na alama inayosomeka ‘skuli’ pembeni yake.

## 1.1h: Mfumo wa elimu ndio wenye tatizo SIO mwanafunzi



Wazazi hawapewi taarifa au kuhusishwa.




Wanafunzi wengi wanaacha skuli.




Ukosefu wa vyoo unaathiri mahudhurio ya watoto wa kike.

**Mfumo wa elimu kama tatizo**



Madarasa yaliosheheni wanafunzi huathiri ubora wa elimu.



Madarasa yasiyofikika



Ukosefu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia



Sera zisizobadilika huwabagua baadhi ya wanafunzi



Ufundishaji duni unasababisha mahitaji ya wanafunzi yasizingatiwe

[Maelezo ya picha: Picha inaonesha mifano minane tofauti ya mfumo wa elimu kama ni tatizo. Kuanzia juu kuelekea kulia:]

Mfano wa kwanza unamuonesha mtoto wa kiume aliyevaa sare ya skuli, amechukua mkoba wa skuli huku akipanda ngazi. Neno 'SEKONDARI' limeandikwa juu ya ngazi. Watoto watatu wamesimama chini ya ngazi. Watoto hao ni pamoja na mtoto mmoja wa kiume akiangalia juu upande waliopo watoto wengine wa kiume, mtoto mmoja wa kike ameshika karatasi yenye maandishi, akiangalia chini na akionekana mwenye huzuni. Mtoto mmoja wa kiume amevaa miwani myeusi, ameshika fimbo na anaangalia upande mwengine. Neno 'MSINGI' limeandikwa chini ya ngazi.

Mfano wa pili unawaonesha watoto saba, wa kike na kiume akiwemo mmoja mwenye gongo la kutembelea na mwengine mwenye ulemavu wa ngozi, wamesimama kwenye foleni wakisubiri kutumia choo. Jengo la choo ni chakavu. Upande wa kushoto, kuna mtoto anafanya haja ndogo kichakani. Jengo la skuli lipo kwa nyuma.

Mfano wa tatu unamuonesha mtoto wa kiume aliyekaa kwenye kitimwendo, akiangalia chini. Kuna ngazi ndefu nyuma yake ambayo inaelekea kwenye mlango wa kuingilia darasani. Kupitia mlangoni anaonekana mwalimu anasomesha.

Mfano wa tano unamuonesha mwanamke aliyesimama mbele ya wanafunzi ambao wamekaa kwenye madawati. Anaashiria juu, anazungumza huku akiwa amewaelekezea mgongo. Mbele ya darasa kuna mwanafunzi mmoja ambae anaangalia nje ya darasa kupitia dirishani na mwengine amelaza kichwa chake kwenye mikono yake.

Mfano wa tano unaonesha vitabu vitatu vilivyowekwa pamoja, rula, penseli na kalamu na kifutio, vyote vikiwa vimezungushiwa duara na mstari uliopita katikati.

Mfano wa sita unamuonesha mwanamke aliyevaa kwa umaridadi amesimama nje ya jengo la skuli akiashiria upande mwengine mbali na skuli. Mtoto wa kike aliyevaa kanzu ya rangi ya zambarau na viatu vya kandambili, akiwa amechukua begi anangalia chini huku akiondoka eneo la skuli. Anaonekana mwenye huzuni. Upande wa nyuma kuna mtoto wa kike na wa kiume waliovalia sare za skuli wanazungumza.

Mfano wa saba unaonesha darasa lililosheheni wanafunzi wengi wakiwa wamebanana katika safu. Mwalimu anaonekana kwa mbali mbele ya darasa akiashiria maandishi kwenye ubao. Kuta za skuli na madirisha yapo katika hali ya uchakavu.

Mfano wa nane unaonesha picha mbili zikiwa zimetenganishwa na mstari mwekundu. Picha ya upande wa kushoto inaonesha jengo likiwa na maandishi SERA ZA ELIMU ubavuni kwake. Lipo nyuma ya uzio wa waya. Kupitia dirishani yanaonekana marundo ya karatasi zilizoparaganyika. Picha ya upande wa kulia inamuonesha mwanamme na mwanamke wakiwa nje ya nyumba ilioezekwa kwa nyasi. Wamenyoosha mikono yao juu kama kwamba kuna kitu hawakifahamu. Nje ya nyumba kuna mtoto mwenye mguu mmoja aliyelala kwenye mkeka.

## 1.1i: Mkabala wa njia pacha

**Lenga katika mfumo:**
Kuhakikisha mazingira ya kufundishIa na kujifunzia, mitazamo na mbinu inazingatia uanuwai na kukuza ujumuishaji. Kuondoa vikwazo

**Lenga kwa mwanafunzi:**
Kuheshimu Mawazo yao na kuwapatia msaada stahiki kwa kuwa ni haki yao. Hii itapelekea kuwezeshwa kupitia uwepo, ushiriki na mafanikio.





**Elimu mjumuisho =**
Kukubali utofauti

[Maelezo ya picha 1 (Lenga katika mfumo): Kuna watu wazima saba waliokaa kuzunguka meza kubwa wakiwemo wanawake 3 na wanaume 4. Mwanamke mmoja amekaa kwenye kitimwendo. Mwanamme yule yule na mwanamke kutoka katika picha iliotangulia nao pia wapo mezani. Baadhi ya watu wanazungumza. Mbele yao juu ya meza kuna karatasi zenye maandishi na kalamu. Nyuma ya chumba, kuna mtu anaandika kwenye ubao. Juu ya ubao Pameandikwa maneno ‘Mafunzo ya Elimu mjumuisho kwa walimu Siku ya 2’.]


[Maelezo ya picha ya 2 (Lenga kwa mwanafunzi): Kuna wanafunzi darasani. Kuna mabango yenye maandishi ukutani. Wamekaa kwenye meza na wanafanya kazi kwa jozi. Kwenye dawati mbele upande wa kushoto mtoto wa kiume asiyeona anatumia nukta nundu na kalamu ya nukta nundu. Ubavuni kwake kuna kijana wa kiume amemuinamia akimhamasisha. Upande wa kulia katika dawati hilo hilo kuna kijana wa kike anamsaidia mwanafunzi mwengine. Nyuma yao mtu yule yule kutoka picha mbili ziliotangulia anaangalia na kutabasamu.]

## 1.1j: Ni muhimu KUANGALIA na KUTAFAKARI kabla ya KUTENDA




**ANGALIA:** kwa mfano, mwanachama wa Jumuiya ya watu wenye ulemavu anatembelea kaya fulani ili kujua kwa nini mwanafunzi hahudhurii skuli.

**TENDA:** Jumuiya ya watu wenye ulemavu imeandaa tukio la kukuza uelewa na imemualika mwanamke ambae ni mfano mzuri wa kuigwa ili azungumze na wazazi katika jamii kuhusu umuhimu wa kuwapeleka watoto wa kike skuli.




**TAFAKARI:** wanachama wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wanakutana na Kamati ya ujumuishi ya skuli ili kujadili ni jinsi gani wanaweza kuwasaidia watoto wa kiume na wa kike kwenda skuli.





[Maelezo ya picha: Mchoro unaonesha picha ya ‘ANGALIA-TAFAKARI-TENDA’ iliopo katikati na picha nyengine kubwa tatu zinazohusiana na picha hiyo zikiwa pembezoni.]


Picha inayofuata baada ya ‘ANGALIA’ inamuonesha mtu aliye na mguu mmoja, aliyevaa suti na anatumia gongo la kutembelea. Amesimama nje ya mlango wa nyumba. Mlango upo wazi. Mwanamke amesimama sawa na mlango anazungumza na mtu aliyesimama. Anaashiria na ameinua kope – kama anayeeleza jambo fulani. Nyuma yake, kupitia mlango ulio wazi mtoto mdogo wa kike aliyevaa kitambaa cha rangi ya pinki kichwani anasafisha sakafu.

Picha inayofuata baada ya ‘TAFAKARI’ inaonesha watu watano waliokusanyika nje chini ya mti, wanne wamekaa kwenye Vigoda na mmoja amesimama. Ni mjumuiko wa wanawake watatu na wanaume wawili. Wanawake wawili wamevaa hijabu, na mwanamme mmoja amevaa kanzu. Watu hawa watano wanamsikiliza mtu anayeongea. Mtu huyo amevaa suti, ana mguu mmoja na anatumia gongo la kutembelea. Amesimama. Pembeni yake kuna chati mgeuzo iliowekwa kwenye stendi ikiwa na mchoro wa watu wawili wadogo – mtoto wa kiume na mtoto wa kike wakiwa ndani ya nyumba

Picha inayofuata ni ‘TENDA’ inaonesha kikundi cha watu wanane wamekusanyika nje. Baadhi ya watu wamekaa, wengine wamesimama. Mwanamke mmoja aliyekaa ana fimbo inayotumiwa na watu wasioona. Mwanamke mwengine aliyesimama anaashiria kwa lugha ya alama akiwasiliana na mtu mzima mwanamme. Mwanamke aliyevaa nguo za kawaida amesimama kwa nyuma. Watu wote wanamuangalia na kumsikiliza mwanamke aliyevaa kwa umaridadi ambae amesimama, anatabasamu, na anazungumza kwa kutumia kipaza sauti. Mkono wake amemzungushia mtoto mdogo wa kike aliyevaa kanzu ya rangi ya zambarau na viatu vya kandambili akiwa amechukua begi. Yule mtoto anamuangalia huku akitabasamu. Mtu aliyevaa suti mwenye mguu mmoja amekaa juu ya kiti ubavuni mwa mwanamke mwenye kipaza sauti. Gongo la kutembelea limewekwa chini. Nyuma ya picha kunaonekana baadhi ya maduka, msikiti, watu wanatembea na wengine wamekaa chini wakionesha bidhaa mbalimbali.]

## 1.1k: Kutambua rasilimali zilizopo katika jamii

Tunaweza kutumia rasilimali zilizopo katika jamii kusaidia kamati ya elimu mjumuisho ya skuli kusaidia kuongeza uelewa kuhusu elimu mjumuisho na kuleta mabadiliko.



[Maelezo ya picha; Katikati ya karatasi kuna maduara matatu yaliochorwa kwa mkono yaliopangwa katika mpangilio wa pembe tatu. Duara la kwanza upande wa kushoto limeandikwa "watu". Jengine limeandikwa "jumuiya" ndani yake na la tatu limeandikwa "rasilimali vitu". Maduara matatu yameunganishwa pamoja kwa mistari myeusi.]

Pembezoni mwa duara la "watu" kuna maduara manne madogo yaliyounganishwa pamoja kwa mstari mweusi. Katika moja ya maduara haya kuna mzee aliyeshika fimbo na chini yake ndani ya duara pameandikwa "Bw. P. mwalimu mstaafu" na chini ya maneno haya kwenye mabano pameandikwa "anasaidia kuzungumza na wazazi". Duara jengine dogo lina picha ya kijana wa kiume anaetumia cherehani na chini yake pameandikwa "Bw. K mshoni". Duara jengine dogo lina picha ya msikiti na maneno "Imamu Msikitini". Katika duara jengine dogo lililounganishwa na duara la watu kuna picha ya kibanda kilichoezekwa bati. Nje ya kibanda kuna watu wamekaa kuzunguka meza. Wawili wanazungumza na mwengine amekaa anakula. Nyuma yake kuna birika jikoni inayochemka.

Pemebzoni mwa duara la "jumuiya" kuna maduara matatu madogo yaliyounganishwa na duara kubwa kwa mstari mweusi. Duara dogo la kwanza lina picha ya dereva wa pikipiki ya maringi matatu (bajaji) chini yake pameandikwa "Chama cha waendesha bajaji". Duara jengine dogo lina picha ya kikundi cha wanawake waliokaa wanazungumza. Chini yake pameandikwa "Jumuiya ya wanawake wa mtaani". Katika duara dogo la tatu pameandikwa "Kikundi cha Vijana" na chini yake kwenye mabano pameandikwa "inasaidia kusambaza machapisho".

[Pembezoni mwa duara la rasilimali vitu kuna maduara sita madogo yaliounganishwa na duara kubwa kwa mstari mweusi. Katika duara la mwanzo kuna picha ya skuli ikiwa na maneno "Madrasa". Duara jengine dogo lina picha ya mwanamke anayeuza matunda na mboga chini yake pameandikwa "Soko la Mboga" na maandishi "miche kwa ajili ya skuli" yakiwa katika mabano.  Duara jengine dogo lina picha ya jengo lenye madirisha mengi na mnara kubwa wa saa katikati. Nje ya jengo hili kuna bango linalosomeka Chuo Kikuu na mbele yake kuna watu watatu wanazungumza. Duara jengine dogo lina picha ya dereva wa 'bajaji' akiwa na abiria. Chini ya picha hii pameandikwa "madereva 'bajaji'" na neno "usafiri" likiwa katika mabano. Kuna maduara mengine madogo yaliounganiswa na rasilimali vitu – moja lina neno "mto" na picha ya mto na neno jengine "ardhi" limeandikwa ndani.]

## Nyenzo nambari 1.1l: Harakati za utetezi zinaweza kuwa kubwa au ndogo

Utetezi ni **kuchukua hatua ili kuleta mabadiliko.**



Utetezi unaweza kujumuisha harakati za kuzungumza na watu ili kuleta **mabadiliko katika namna ambayo watu wanafikiria (mitazamo)**





Utetezi pia unahusisha **kuwasaidia watu kuunganisha sauti zao, ili walete mabadiliko katika namna ambayo mambo yanafanywa (utekelezaji).**

Maelezo ya picha 1: Watu watatu wamesimama wanazungumza. Mwanamke aliye upande wa kulia anatumia mikono yake kutoa ishara kwa mtu mzima mwanamme anaemuangalia ambae pia anaashiria kwa mikono yake. Mwanamke aliyekaa katikati anasikiliza na kuangalia. Kwa nyuma kuna maduka na msikiti na mtoto wa kike, ambae hajavaa sare za skuli, anamsukuma mtoto wa kiume aliyekaa kwenye kitimwendo.]

[Maelezo ya picha 2: Kikundi cha watu kimekaa katika mtindo wa safu wakimuelekea Spika ambae hayupo katika picha. Katika kikundi kuna mwanamke aliyekaa kwenye kitimwendo ambae anaandika, mtu mmoja mwanamme mwenye ulemavu wa ngozi amenyoosha mkono na mwanamke mwengine aliyesimama ambae amenyoosha mkono. Watu wengine wawili wameelekeana wanazungumza jambo. Neno BUNGE limeandikwa kwa herufi kubwa chini ya picha.]

## 1.1m: Uhamaji jumuishi huanzia nyumbani

Familia, nyumbani na jamii vinabaki kuwa ni nyenzo muhimu mwanafunzi anapohama baina ya ngazi tofauti za elimu



Maelezo ya picha: Picha inaonesha familia iliyopo katikati na majengo manne yaliyopo kila pembe, na njia pamoja na mishale ikiunganisha majengo na familia. Familia inajumuisha mtoto mdogo wa kike, mtoto mkubwa wa kike na mtoto mkubwa wa kiume, kikongwe aliyeshika fimbo ya kutembelea, mwanamke na mwanamme mtu mzima. Maneno ‘Familia na nyumbani’ yameandikwa chini ya kikundi cha wanafamilia. Juu ya picha upande wa kushoto, kuna jengo limeandikwa ‘skuli ya maandalizi’. Mtoto mdogo wa kike akiwa ameushika mkono wa mtoto mkubwa wa kike wanatembea katika njia kuelekea ‘skuli ya maandalizi’. Kuna mshale uliopinda kutoka skuli ya maandalizi ukielekea juu pembe ya kulia ambako kuna jengo lililoandikwa ‘skuli ya msingi’. Picha nyengine ya mtoto mdogo wa kike ambae amekua sasa anaonekana akitembea kutoka katika familia yake akielekea skuli ya msingi; ameshika fimbo ndefu. Kuna mshale uliopinda kutoka kwenye skuli ya msingi kuelekea chini pembe ya kulia ambako kuna jengo lililoandikwa ‘skuli ya sekondari’. Picha nyengine ya mtoto huyo huyo akiwa amekua zaidi anaonekana akitembea kutoka katika familia yake kuelekea skuli ya sekondari; ameshika fimbo ndefu. Mwisho, kuna mshale uliopinda kuelekea chini pembe ya kushoto ambako kuna jengo lililoandikwa ‘chuo kikuu’. Mwanamke kijana, akiwa ameshika fimbo ndefu, anatembea kwenye njia kutoka kwao akielekea chuo kikuu.]

## 1.1n: Majukumu tofauti ya Jumuiya za Watu wenye Ulemavu katika Utetezi wa Elimu Mjumuisho

Kushawishi kwa kutumia sera ili kufanya maamuzi na kupata mabadiliko chanya.



Kuangalia, kukusanya taarifa ili kujenga ushahidi kwa ajili ya kuleta mabadiliko



Kufuatilia na kuwezesha hatua za kuleta mabadiliko katika elimu mjumuisho.




Kujenga ushirikiano madhubuti na mitandao ili kuongeza uelewa kwa ajili ya kuleta mabadiliko chanya.



Kukuza uelewa kuhusu mabadiliko yanayohitajika katika elimu mjumuisho.



[Maelezo ya picha 1: Kuna watu watano waliokaa katika chumba. Kuna kalenda ukutani. Upande wa kulia kuna mtu mzima mwanamme aliyevaa kwa umaridadi ambae amekaa nyuma ya dawati likiwa na karatasi juu yake. Juu ya dawati kuna maneno yanayosomeka 'Afisa Elimu Wilaya'. Anasikiliza. Kuna watu wanne waliokaa juu ya viti wakimuelekea Afisa Elimu. Karibu na Afisa Elimu kuna mwanamke aliyevaa kanzu ndefu nadhifu akiwa ameshika fimbo ndefu nyeupe, akiashiria na kuelezea jambo kwa Afisa Elimu. Ameshika baadhi ya nyaraka rasmi za Serikali zikiwa na nembo juu yake. Karibu yake kuna mtoto wa kiume aliyeshika fimbo nyeupe pamoja na mwanamme na mwanamke mtu mzima. Wanatabasamu.]

[Maelezo ya picha 2: Mtu mzima mwanamme mwenye mguu mmoja, aiyevaa suti na anatumia gongo la kutembelea. Amesimama nje ya mlango wa nyumba. Mlango umefunguliwa. Mwanamke mtu mzima amesimama nje ya mlango uliofunguliwa akizungumza na nae. Anaongea kwa kuashiria huku nyusi zake zikiwa zimepanda – kana kwamba anaelezea jambo. Nyuma yake, kupitia mlango ulio wazi mtoto wa kike anasafisha sakafu.]

[Maelezo ya picha 3: Kuna watu wengi, wanaume watu wazima, wanawake watu wazima, na watoto wanaofanya kazi pamoja mbele ya jengo la skuli. Mtu mzima mwanamme anasukuma toroli likiwa na mawe makubwa ndani. Baadhi ya watu wanapanga mawe kutengeneza kingo za njia inayoelekea skuli. Mtoto wa kiume aliyekaa kwenye kitimwendo anaonesha wapi mawe yawekwe. Kwa nyuma kuna wanawake wawili watu wazima waliovaa kwa umaridadi wanazungumza. Mtoto wa kiume mwenye fimbo nyeupe anatembea kando ya mwanamke ambae amebeba sanduku la chupa za maji.]

[Maelezo ya picha 4: kuna watu tisa wamekaa kwenye mabenchi kwa mtindo wa nusu duara katika chumba chenye madirisha matatu upande wa nyuma. Kupitia madirishani unaweza kuona baadhi ya majengo ambayo yanaonekana kama ni majengo ya skuli. Waliomo katika kundi ni mtu mzima mwanamme aliyekaa kwenye kitimwendo, mtu mzima wa makamo mwanamme akiwa na fimbo ya kutembelea na mtoto wa kike aliyevaa sare ya skuli ambae ana mguu mmoja na anatumia gongo la kutembelea, ukijumlisha wanawake wengine watatu na mwanamme mtu mzima. Mwanamke aliyevaa nguo za kawaida anazungumza. Pembeni yake, kuna mtoto mdogo wa kiume aliyekaa kwenye benchi ambae amevaa miwani myeusi aliyeshika fimbo ndefu. Watu wote wanamsikiliza mwanamke, na nyuso zao zinaonesha hali ya taharuki.]

[Maelezo ya picha 5: kikundi cha watu wanane wamekusanyika nje. Baadhi yao wamekaa, na wengine wamesimama. Mwanamke mmoja aliyekaa ana fimbo inayotumiwa na wasioona. Mwanamke mwengine aliyesimama anatumia mikono kuashiria akiwasiliana na mtu mzima mwanamme. Watu wote wanamuangalia na kumsikiliza mwanamke aliyevaa kwa unadhifu ambae amesimama, akitabasamu, na anazungumza kwa kutumia kipaza sauti. Mkono wake amemzungushia mtoto mdogo wa kike aliyevaa kanzu ya rangi ya zambarau na kandambili ambae ameshika begi. Mtoto anaangalia huku akitabasamu. Mwanamme aliyevaa suti mwenye mguu mmoja amekaa juu ya kiti kando ya mwanamke aliyeshika kipaza sauti. Gongo la kutembelea imewekwa chini. Kwa nyuma yanaonekana maduka, msikiti, watu wanatembea na wengine wamekaa chini wakinadi bidhaa zao.]

# Nyenzo namabri 1.3: MUONGOZO WA UTETEZI: Kusaidia jumuiya za watu wenye ulemavu kufanya utetezi wa elimu mjumuisho

## Lengo lake ni nini?

Muongozo huu umekusanya mambo yote muhimu tuliyojifunza ambayo yatatusaidia kuwa watetezi wazuri wa elimu mjumuisho. Unaeleza kwa muhutasari tulichojadili kuhusu elimu mjumuisho na inamaanisha nini kuwa mtetezi wa elimu mjumuisho. Pia unatukumbusha kuhusu jukumu muhimu ambalo Jumuiya za watu wenye ulemavu zinaweza kutekeleza, jinsi gani tunaweza kujifunza kupitia tunachofanya na kuendeleza mabadiliko tuliochangia kuyaleta. Muongozo pia unajadili jumbe mahususi ambazo ni muhimu kwa ajili ya kukuza uelewa kuhusu elimu mjumuisho na kusaidia watu kufahamu elimu mjumuisho.

## Kuna maudhui gani katika muongozo wa utetezi?

**Mwanzo kuna utangulizi mfupi unaoelezea lengo la muongozo na unatumikaje. Kisha, unafuatiwa na sehemu 5.**

### Sehemu ya 1: Nini maana ya utetezi wa elimu mjumuisho?

Sehemu hii inaelezea nini maana ya utetezi, nani anaweza kuwa mtetezi na mtetezi hufanya nini. Pia inaelezea inamaanisha nini kuwa mtetezi wa elimu mjumuisho.

### Sehemu ya 2: Jukumu la Jumuiya za watu wenye ulemavu katika kufanya utetezi wa elimu mjumuisho.

Sehemu hii inajadili majukumu muhimu ya utetezi ambayo Jumuiya za watu wenye ulemavu kuanzishwa na zinaweza kutekeleza kuanzisha na kuendeleza elimu mjumuisho. Inaeleza:

- Kila jukumu linahusu nini
- ujuzi upi na maarifa gani yanayohitajika ili kutekeleza jukumu hili ipasavyo
- nyenzo zipi zitasaidia utekelezaji wa jukumu hili
- wakati gani tunaweza kutekeleza jukumu hili

Haya ni majukumu matano ya msingi ambayo yameelezwa katika sehemu hii

- Kutafuta na kukusanya taarifa ili kujenga ushahidi kwa ajili ya kuleta mabadiliko
- Kujenga ushirikiana imara ili kujenga ushirikiano imara na mitandao kwa ajili ya kuleta mabadiliko
- Kukuza uelewa kuhusu mabadiliko gani yanahitajika kwa ajili ya elimu mjumuisho
- Kutumia sera kushawishi maamuzi kwa ili kuleta mabadiliko.
- Kufuatilia na kusaidia mchakato wa mabadiliko kwa ajili ya elimu mjumuisho

## Sehemu ya 3: Ujumbe muhimu kwa ajili ya utetezi wa elimu mjumuisho

Sehemu hii inatukumbusha kwamba watu wana mawazo tofauti na uelewa kuhusu elimu mjumuisho. Kama watetezi tunapaswa kushirikiana ili kujenga uelewa kwa watu juu ya maana ya elimu mjumuisho na tujitahidi, ili kwa umakini tujenge mitazamo sahihi kuhusu elimu mjumuisho dhidi ya mitazamo isiyo sahihi.

- Jumbe muhimu kuhusu elimu mjumuisho ambazo tunataka kuziwasilisha.
- Ujumbe upi mzuri zaidi kuuwasilisha katika hali fulani (mf. kuwaelezea wazazi wa watoto wenye ulemavu kuhusu mkabala wa njia pacha ili kuwafanya wajiamini kuwapeleka watoto wao skuli)
- Mbinu ipi nzuri zaidi ya kuwasilisha ujumbe kwa watu/kikundi tunaowasiliana nao (mf. kutumia picha kufikisha ujumbe kwa wanajamii wenye kiwango cha chini cha elimu)

Inatukumbusha kuhusu jumbe 4 muhimu tulizojifunza:

- Watoto wanapotengwa au hawaendi skuli, mfumo ndio tatizo sio mwanafunzi.
- Elimu mjumuisho inamaanisha watoto wote wanakuwepo, wanashiriki na wanafanikiwa.
- Kuanzisha na kuimarisha elimu mjumuisho inamaanisha kukuza uwezo wa wadau wote kutambua na kuondoa vikwazo vinavyozuia ujumuishwaji.
- Kusaidia mfumo na mwanafunzi yote mawili ni muhimu katika elimu mjumuisho.

## Sehemu ya 4: Kuendeleza mabadiliko kupitia utetezi wa elimu mjumuisho

Sehemu hii inaelezea tunahitaji nini ili kuendeleza kazi yetu ya utetezi. Inatukumbusha kwamba kuanzisha elimu mjumuisho ni jambo linalochukuwa muda, kwa hivyo tunahitaji kuendeleza kazi yetu ya utetezi. Inajadili mikakati mikuu tunayoweza kuitumia kutekeleza hilo. Tutajadili haya kwa kina tutakapojifunza Moduli 4 – hii ni mikakati ambayo tutaijadili.

- Kuangalia na kutafakari kuhusu vikwazo vya elimu mjumuisho
- Kuendelea kukuza uelewa kuhusu elimu mjumuisho
- Kuimarisha ushirikiano katika jamii
- Kuendelea kushawishi sera ili kusaidia elimu mjumuisho.
- Kuimarisha harakati zinazokuza elimu mjumuisho
- Kuendelea kujifunza kama watetezi.

## Sehemu ya 5: Baadhi ya nyenzo muhimu

Sehemu hii ina nyenzo mbalimbali ambazo huenda tukataka kuzitumia katika kazi yetu ya utetezi – kama vile viunganishi kwa ajili ya sera muhimu, mifano (templates) tunayoweza kuitumia kwa ajili ya kupanga na kuripoti kazi yetu; miongozo ya kutusaidia; na viunganishi vya kutuunganisha na taasisi nje ya nchi ambazo tunaweza kujifunza kwao.

# Nyenzo nambar 2.1: Muongozo wa kuandaa mabango/kupeana taarifa kuhusu mafanikio.

Tungependa uandae bango la kawaida tu linalooonesha mafanikio na maendeleo uliofikia kama Jumuiya ya watu wenye ulemavu katika kutetea elimu mjumuisho katika Shehiya yako kwa miaka 2 iliyopita.

Bango/mabango yatengenezwe kwa kutumia karatasi ya chati mgeuzo na yanaweza kujumuisha:

- Michoro ya kawaida au maumbo
- Picha za shughuli mlizofanya zilizochapishwa kwa rangi na sentensi zinazoelezea kazi yenu ya utetezi

Kama hakuna nafasi ya kutosha ya kuingiza kila kitu katika chati mgeuzo, unaweza kuongeza karatasi zaidi.

## Kuandaa bango lako

Kama JWU, tafakari kuhusu unachotaka kuweka katika bango/mabango yenu. Huenda ukataka kuzingatia maswali yafuatayo:

- Shughuli gani umekuwa unafanya ili kutetea elimu mjumuisho katika wilaya yako?
- Umeongeza ujuzi gani na uzoefu upi katika miaka miwili iliyopita?
- Umebaini mabadiliko gani katika wilaya yako yaliyotokana na kazi yako ya utetezi?
- Changamoto zipi ulizozipitia na jinsi gani ulizitatua? (Hivi sio vikwazo vya elimu mjumuisho, lakini ni changamoto katika kutekeleza kazi yako ya utetezi wa elimu mjumuisho)
- Mnafanyaje kazi kwa kushirikiana ili kukuza elimu mjumuisho? (Hii ni pamoja na kushirikiana na Kamati ya Skuli ya Elimu mjumuisho, serikali ya mtaa na wadau wasio wa serikali, viongozi wa mtaa n.k.)
- Una mipango gani ya kuendeleza kazi yako ya utetezi katika siku zijazo?

Jadili nukta muhimu zaidi za kuziingiza katika mabango yako na jinsi gani utazifafanua nukta hizo. Hutoweza kuweka kila kitu, lakini weka kwa ufupi ‘sehemu ndogo tu’ ya kazi yako.

Kumbuka picha mara nyingi hutoa taarifa zaidi kuliko maneno!

Chagua picha ambazo unataka kuzichapisha kwa ajili ya bango lako. Iwapo huwezi kuchapisha picha katika ngazi ya wilaya, kutakuwa na fursa ya kuchapisha katika siku ya mwanzo ya mafunzo katika mafunzo ya ngazi ya taifa.

## Nyenzo nambari 3.1: Majukumu ya Jumuiya za Watu wenye Ulemavu katika Kutetea Elimu Mjumuisho

### A. Kushawishi kwa kutumia sera ili kufanya maamuzi na kupata mabadiliko chanya.



[Maelezo ya picha: Kuna watu watano waliokaa katika chumba. Kuna kalenda ukutani. Upande wa kulia kuna mtu mzima mwanamme aliyevaa kwa umaridadi ambae amekaa nyuma ya dawati likiwa na karatasi juu yake. Juu ya dawati kuna maneno yanayosomeka ‘Afisa Elimu Wilaya’. Anasikiliza. Kuna watu wanne waliokaa juu ya viti wakimuelekea Afisa Elimu. Karibu na Afisa Elimu kuna mwanamke aliyevaa kanzu ndefu nadhifu akiwa ameshika fimbo ndefu nyeupe, akiashiria na kuelezea jambo kwa Afisa Elimu. Ameshika baadhi ya nyaraka rasmi za Serikali zikiwa na nembo juu yake. Karibu yake kuna mtoto wa kiume aliyeshika fimbo nyeupe pamoja na mwanamme na mwanamke mtu mzima. Wanatabasamu.]

**B. Kutafuta na kukusanya taarifa kwa ajili ya kuandaa ushahidi kwa ajili ya mabadiliko.**




[Maelezo ya picha: Mtu mzima mwanamme mwenye mguu mmoja, aliyevaa suti na anatumia gongo la kutembelea. Amesimama nje ya mlango wa nyumba. Mlango umefunguliwa. Mwanamke mtu mzima amesimama nje ya mlango ulio wazi akizungumza na mtu. Anaongea kwa kuashiria huku nyusi zake zikiwa zimepanda – kama kwamba anaelezea jambo. Nyuma yake, kupitia mlango ulio wazi mtoto wa kike anasafisha sakafu.]

**C. Kujenga ushirikiano imara na mitandao ili kuleta mabadiliko.**



[Maelezo ya picha: kuna watu tisa wamekaa kwenye mabenchi kwa mtindo wa nusu duara katika chumba chenye madirisha matatu upande wa nyuma. Kupitia madirishani unaweza kuona baadhi ya majengo ambayo yanaonekana kama ni majengo ya skuli. Waliomo katika kundi ni mtu mzima mwanamme aliyekaa kwenye kitimwendo, mtu mzima wa makamo mwanamme akiwa na fimbo ya kutembelea na mtoto wa kike aliyevaa sare ya skuli ambae ana mguu mmoja na anatumia gongo la kutembelea, ukijumlisha wanawake wengine watatu na mwanamme mtu mzima. Mwanamke aliyevaa nguo za kawaida anazungumza. Pembeni yake, kuna mtoto mdogo wa kiume aliyekaa kwenye benchi ambae amevaa miwani myeusi aliyeshika fimbo ndefu. Watu wote wanamsikiliza mwanamke, na nyuso zao zinaonesha hali ya taharuki.]

**D. Kukuza uelewa kuhusu mabadiliko yanayohitajika kwa ajili ya elimu mjumuisho.**



[Maelezo ya picha 5: kikundi cha watu wanane wamekusanyika nje. Baadhi yao wamekaa, na wengine wamesimama. Mwanamke mmoja ameshika fimbo inayotumiwa na wasioona. Mwanamke mwengine aliyesimama anatumia mikono kuashiria akiwasiliana na mtu mzima mwanamme. Watu wote wanamuangalia na kumsikiliza mwanamke aliyevaa kwa unadhifu ambae amesimama, akitabasamu, na anazungumza kwa kutumia kipaza sauti. Mkono wake amemzungushia mtoto mdogo wa kike aliyevaa kanzu ya rangi ya zambarau na kandambili aliyeshika begi. Mtoto anaangalia huku akitabasamu. Mwanamme aliyevaa suti mwenye mguu mmoja amekaa juu ya kiti kando ya mwanamke aliyeshika kipaza sauti. Fimbo ya kutembelea imewekwa chini. Kwa nyuma yanaonekana maduka, msikiti, watu wanatembea na wengine wamekaa chini wakinadi bidhaa zao.]

**E. Kufuatilia na kusaidia mchakato wa mabadiliko katika elimu mjumuisho**



[Maelezo ya picha: Kuna watu wengi, wanaume watu wazima, wanawake watu wazima, na watoto wanaofanya kazi pamoja mbele ya jengo la skuli. Mtu mzima mwanamme anasukuma toroli likiwa na mawe makubwa ndani. Baadhi ya watu wanapanga mawe kutengeneza kingo za njia inayoelekea skuli. Mtoto wa kiume aliyekaa kwenye kitimwendo anaelekeza wapi mawe yawekwe. Kwa nyuma kuna wanawake wawili watu wazima waliovaa kwa umaridadi wanazungumza. Mtoto wa kiume mwenye fimbo nyeupe anatembea kando ya mwanamke ambae amebeba sanduku la chupa za maji.]

## Nyenzo nambari 4.2: Mikakati muhimu ya kuendeleza kazi ya utetezi katika elimu mjumuisho

| |
|---|
| Kujenga uwezo wa ushawishi katika ngazi ya mtaa (mf. kuupatia mafunzo uongozi wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu) |
| Kuwapatia mafunzo watetezi jamii na wanaharakati wa elimu mjumuisho |
| Kushirikiana na skuli, serikali ya mtaa, na wadau wengine muhimu |
| Kuwabaini na kushirikiana na watu mashuhuri katika ngazi ya mtaa |
| Kushirikiana na kamati ya skuli ya elimu mjumuisho |
| Kushirikiana na serikali ya mtaa |
| Kuanzisha vikundi vya ushirikiano vya ngazi ya mtaa kama vile vikundi vya kusaidiana vya wazazi |
| Kutambua mali (na rasilimali) zinazopatikana katika jamii |
| Kukuza uelewa kuhusu elimu mjumuisho na kusaidia kuondoa mitazamo hasi katika jamii |
| Kutumia sera kushawishi mabadiliko ili kushawishi mabadiliko |

| |
|---|
| Kuendesha kampeni ya utetezi ngazi ya taifa |
| Shughuli za kiuchumi/kushirikiana na wafanya biashara wa mtaani kuchangisha fedha kwa ajili ya elimu mjumuisho |
| Kuendelea kutafakari kuhusu ulichojifunza na jinsi ya kutumia mafunzo kurekebisha mipango ya utetezi |
| Kuwatambua wanafunzi wenye ulemavu walio nje ya skuli na kutoa vifaa saidizi |
| *Blank for additional strategy* |
| *Blank for additional strategy* |

# Nyenzo nambari 4.4: Sehemu za maigizo zinazoonesha changamoto za uendelevu katika elimu mjumuisho

**Hali ya 1: Mabadiliko katika uongozi wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu**

Kumeakuwa na mabadiliko katika uongozi wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu. Kuna viongozi wapya waliochaguliwa ambao hawana taarifa au hawajawahi kupata mafunzo kuhusu elimu mjumuisho na hawafahamu elimu mjumuisho inatekelezwaje. Wanadhani kuna rasilimali nyingi na msaada wa fedha ambao utahitajika kabla ya skuli hazijawa jumuishi. Kuna hatari ya kwamba uwezo (ujuzi na maarifa) kuhusu elimu mjumuisho ambao Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu ilishaanza kuyajenga na kuna hofu yakupotea chini ya uongozi mpya. Pia, uongozi mpya hauoni umuhimu wa kutenga muda 'kutafakari juu ya mafunzo' na kutumia nyenzo kama vile duara la 'angalia – tafakari - tenda' katika kusaidia kufanya maamuzi kuhusu mbinu ipi inaleta tija na jinsi gani walete mabadiliko.

Mnapojiandaa kwa igizo lenu zingatieni yafuatayo:

- Hali ikoje na kuna changamoto gani zinazozuia uendelevu?
- Nani atahusika? (Nani katika kikundi chenu atacheza nafasi ipi)
- Vipi unaweza kuonesha kwa uwazi hali halisi na changamoto kupitia igizo?
- Taarifa zipi ambazo unaweza kuongezea ili kufanya igizo lionekane lina uhalisia na sahihi?

Hakikisha kwamba igizo lenu linaonesha hali halisi na usitishe igizo lenu katika kipengele cha changamoto bila ya kutatua changamoto hizo. Kusudio ni kwamba hali inaachwa kama ilivyo, na hadhira inakaribishwa kushauri mikakti ya kusaidia kutatua tatizo.

**Hali ya 2: Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu haiwezi kuikabili ipasavyo serikali ya mtaa.**

Jumuiya ya watu wenye ulemavu inashindwa kuikabili ipasavyo mamlaka yenye dhamana ya kusimamia elimu katika eneo husika. Kwa upande mwengine jumuiya inatambua kuwa ni muhimu kujenga uhusiano na serikali ya mtaa ili kuondoa vikwazo vya elimu mjumuisho katika wilaya nzima, hata hivyo wanahisi kwamba hawana nguvu katika hatua za kufanya maamuzi na Afisa elimu wilaya hawapi mud awa kutosha au hawapi kupaumbele. Jumuiya ya watu wenye ulemavu inatambua kwamba kuna baadhi ya sera nzuri za elimu mjumuisho ambazo zipo lakini pia inatambua kwamba hazitekelezwi na inafikiri afisi ya elimu wilaya inahitaji kuchukua hatua kwa jambo hilo. Kwa upande mwengine, serikali ya mtaa imezidiwa na imekosa uwezo na nyenzo na hivyo haioni haja ya kushughulika na elimu mjumuisho.

Mnapojiandaa kwa igizo lenu zingatieni maswali yafuatayo:

- Hali ikoje na kuna changamoto gani zinazozuia uendelevu?
- Nani atahusika? (Nani katika kikundi chenu atacheza nafasi ipi)
- Vipi unaweza kuonesha kwa uwazi hali halisi na changamoto kupitia igizo?
- Taarifa zipi ambazo unaweza kuongezea ili kufanya igizo lionekane lina uhalisia na sahihi?

Hakikisha kwamba igizo lenu linaonesha hali halisi na usitishe igizo lenu katika kipengele cha changamoto bila ya kutatua changamoto hizo. Kusudio ni kwamba hali inaachwa kama ilivyo, na hadhira inakaribishwa kushauri mikakti ya kusaidia kutatua tatizo.

**Hali ya 3: Ujumbe usio sahihi (uliopotoshwa) kuhusu elimu mjumuisho unaenezwa na watu mashuhuri katika jamii**

Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu imefanya Shughuli ya kutambua rasilimali zilizomo katika jamii ili kuwatambua watu mashuhuri katika jamii ili wasaidie kazi ya utetezi wa elimu mjumuisho. Hata hivyo, mmoja au wawili kati ya watu hawa hawatoi taarifa sahihi kuhusu elimu mjumuisho na wakati mwengine wamekua wakishauri watoto wenye ulemavu wapelekwe katika skuli maalumu. Hawakubaliani moja kwa moja kuwa skuli zilizopo zinaweza kuwezeshwa ili ziwe jumuishi. Taarifa hizi mchanganyiko zinaleta mkanganyiko kwa wazazi na walezi wa watoto wenye ulemavu, na hawajui wafanyeje.

Mnapojiandaa kwa igizo lenu zingatieni maswali yafuatayo:

- Hali ikoje na kuna changamoto gani zinazozuia uendelevu?
- Nani atahusika? (Nani katika kikundi chenu atacheza nafasi ipi)
- Vipi unaweza kuonesha kwa uwazi hali halisi na changamoto kupitia igizo?
- Taarifa zipi ambazo unaweza kuongezea ili kufanya igizo lionekane lina uhalisia na sahihi?

Hakikisha kwamba igizo lenu linaonesha hali halisi na usitishe igizo lenu katika kipengele cha changamoto bila ya kutatua changamoto hizo. Kusudio ni kwamba hali inaachwa kama ilivyo, na hadhira inakaribishwa kushauri mikakti ya kusaidia kutatua tatizo.

**Hali ya 4: Kamati ya Elimu mjumuisho ya skuli haifanyi kazi ipasavyo.**

Jumuiya ya watu wenye ulemavu imejaribu kuikabili kamati ya ujumuishi ya skuli (SIT) kujadili vikwazo vinavyokabili elimu mjumuisho katika jamii na wanapanga kuendesha harakati za pamoja ili kuondoa vikwazo hivi. Hata hivyo, Jumuiya ya watu wenye ulemavu imebaini kwamba kamati ya ujumuishi haifanyi kazi ipasavyo na haifuati muongozo ulioyolewa kwa ajili ya kuanzisha na kusimamia kamati ya elimu mjumuisho. Kamati imekutana mara mbili tu na hata hivyo, hakukuwepo na uwakilishi mzuri kutoka katika jamii inayozunguka skuli. Kamati imeshindwa kupanga vipaumbele na kulikuwa na mivutano ndani ya kamati. Mmoja au watu wawili walitawala kikao na hawakuwaruhusu watu wengine kuzungumza. Aidha, jumuiya ya watu wenye ulemavu inadhani kwamba kamati ya elimu mjumuisho haitilii maanani jukumu lake, haisimamii kikundi ipasavyo na inabidi ibadilishwe.

Mnapojiandaa kwa igizo lenu zingatieni maswali yafuatayo:

- Hali ikoje na kuna changamoto gani zinazozuia uendelevu?
- Nani atahusika? (Nani katika kikundi chenu atacheza nafasi ipi)
- Vipi unaweza kuonesha kwa uwazi hali halisi na changamoto kupitia igizo?
- Taarifa zipi ambazo unaweza kuongezea ili kufanya igizo lionekane lina uhalisia na sahihi?

Hakikisha kwamba igizo lenu linaonesha hali halisi na usitishe igizo lenu katika kipengele cha changamoto bila ya kutatua changamoto hizo. Kusudio ni kwamba hali inaachwa kama ilivyo, na hadhira inakaribishwa kushauri mikakti ya kusaidia kutatua tatizo.

**Hali ya 5: Matatizo makubwa (mf. umasikini au ukosefu wa ajira) yanafanya isiwezekane kushughulikia elimu mjumuisho.**

Jumuiya ya watu wenye ulemavu imefanya kazi kubwa kuzungumza na wazazi na walezi juu ya umuhimu wa kuwapeleka watoto wao skuli. Hata hivyo, wazazi na walezi wametingwa zaidi na harakati za kutafuta chakula kwa ajili ya familia na mahitaji mengine ya kila siku kiasi kwamba hawafikirii elimu mjumuisho. Matokeo yake wanafunzi hawahudhurii skuli kwa kipindi kirefu. Kwa wale ambao wanatamani au wanaweza kuwapeleka watoto wao skuli, wamekatishwa tamaa kwa sababu hawawezi kumudu gharama za kuwapeleka watoto wao skuli.

Mnapojiandaa kwa igizo lenu zingatieni maswali yafuatayo:

- Hali ikoje na kuna changamoto gani zinazozuia uendelevu?
- Nani atahusika? (Nani katika kikundi chenu atacheza nafasi ipi)
- Vipi unaweza kuonesha kwa uwazi hali halisi na changamoto kupitia igizo?
- Taarifa zipi ambazo unaweza kuongezea ili kufanya igizo lionekane lina uhalisia na sahihi?

Hakikisha kwamba igizo lenu linaonesha hali halisi na usitishe igizo lenu katika kipengele cha changamoto bila ya kutatua changamoto hizo. Kusudio ni kwamba hali inaachwa kama ilivyo, na hadhira inakaribishwa kushauri mikakti ya kusaidia kutatua tatizo.

**Hali ya 6: Baadhi ya wanafunzi wanaacha skuli miezi michache baada ya kuandikishwa.**

Harakati za kukuza uelewa kuhusu elimu mjumuisho ambazo ziliendeshwa na jumuiya ya watu wenye ulemavu katika jamii zimesaidia kuwahamasisha wazazi zaidi kufahamu kwamba watoto wao wenye ulemavu wana haki ya kwenda skuli na wanaweza kujifunza na kutumia vipaji vyao. Hata hivyo, miezi michache baadae baadhi ya wanafunzi wameanza kuacha skuli kwa sababu hawajapatiwa msaada wanaouhitaji ili waendelee kubaki skuli. Kuna sababu tofauti, baadhi yao wanachokozwa na wanafunzi wengine skuli, wengine wanapata shida sana wakati wa kwenda skuli, na wengine hawasaidiwi na walimu wao kujifunza wanapokuwa darasani na wanaachwa 'wafanye mambo yao' nyuma ya darasa.

Mnapojiandaa kwa igizo lenu zingatieni maswali yafuatayo:

- Hali ikoje na kuna changamoto gani zinazozuia uendelevu?
- Nani atahusika? (Nani katika kikundi chenu atacheza nafasi ipi)
- Vipi unaweza kuonesha kwa uwazi hali halisi na changamoto kupitia igizo?
- Taarifa zipi ambazo unaweza kuongezea ili kufanya igizo lionekane lina uhalisia na sahihi?

Hakikisha kwamba igizo lenu linaonesha hali halisi na sitisha igizo lenu katika kipengele cha changamoto bila ya kuzitatua changamoto hizo. Kusudio ni kwamba hali inaachwa kama ilivyo, na hadhira inakaribishwa kushauri mikakti ya kusaidia kutatua tatizo.

**Hali ya 7: Sera mpya ya utetezi imeandaliwa na shirika mama la jumuia za watu wenye ulemavu.**

Ni nyaraka nzuri lakini bado inahitaji kazi kubwa kutoka kwa shirika mama lenyewe. Baadhi ya vipengele vilivyomo si vya uhalisia. Jumuia za Watu Wenye Ulemavu zinatambua vyema kuwa utetezi ni kiini cha jukumu lao na ni muhimu katika kuongeza ujumuishaji katika mifumo ya elimu, kijamii na kitamaduni. Hata hivyo, sera haielezi jinsi ya kutekeleza mambo hayo bali inaeleza tu nini kifanyike.

- Jumuia za watu wenye ulemavu zinawezaje kusonga mbele kuhusu hili?
- Vipi jumuia zitazungumza na shirika mama kuhusu masuala haya?
- Ni nani wengine wanaopaswa kushirikishwa ili kuwa na majadiliano yenye manufaa kuhusu sera na utekelezaji wake?
- Vipi zitahakikisha zinapata mwongozo wa jinsi ya kufanya utetezi huo?

**Hali ya 8:Watoto watatu waliokuwa nje ya mfumo wa skuli walijiunga na skuli ya msingi mwaka jana.**

Ingawa walikuwa nyuma kielimu, waliweza kuendana na wenzao na kufanya vizuri. Walikuwa tayari kuhamia sekondari na jumuia za watu wenye ulemavu zilifanikiwa kufanya utetezi ili waruhusiwe kupunguziwa ugumu wa mitihani kidogo ili waendelee na masomo. Hata hivyo, mamlaka za Tanzania bara ambazo ndizo zinazohusika na sera kuu kuhusu uhamisho wa wanafunzi hazikuridhika. Ziliruhusu watoto hao waendelee lakini ziliwaambia jumuia za watu wenye ulemavu kuwa haziwezi kufanya maamuzi binafsi na mamlaka za Zanzibar bila kushirikisha bara. Kufanya kazi na mamlaka za bara kuna urasimu na huchukua muda mrefu. Ni rahisi zaidi kufanya kazi na Wizara ya Elimu Zanzibar ambayo inazijua na kuzithamini jumuia za watu wenye ulemavu, na pia inaelewa hali za wanafunzi.

- Ni nani anapaswa kufanya utetezi ili kubadili mfumo wa sera za Tanzania bara, na afanyeje?
- Jumuia za atu wenye ulemavu zinawezaje kushiriki na kushirikisha maarifa yao ya utetezi kwa maafisa wa elimu watakaoshirikiana na maafisa wa Tanzania bara?

**Hali ya 9: Jumui za Watu wenye Ulemavu zinajaribu kufanya kazi kwa ushirikiano lakini changamoto bado zipo.**

Kwanza, kila Jumuia huchangia vizuri katika kupanga lakini wakati wa kuandaa na kutekeleza shughuli, kila moja huhisi kuwa mwenzake ndiye anapaswa kufanya. Pia kuna ajenda binafsi kwenye shehia, mtaa au familia, jambo ambalo husababisha kualikwa kwa watu wasio sahihi kwenye hafla au warsha.Changamoto kubwa zaidi ni katika usimamizi wa fedha: mara nyingi mtu anayezikusanya au kuzisimamia huchukua au "kukopa" fedha kwa ajili yake binafsi au kwa ajili ya jumuia yake. Ni wazi kuwa Jumuia zina sauti yenye nguvu zaidi na zinaweza kuwa na ufanisi zaidi zinaposhirikiana, lakini zinawezaje kushinda changamoto hizi?

- Nini kitatekelezwa ili kukabiliana na changamoto hizi?
- Mfumo utakaoanzishwa utafuatiliwa vipi kuhakikisha unafanya kazi?
- Ni adhabu gani Jumuia au wanachama binafsi watakabiliana nazo endapo watavunja sheria au uaminifu?